# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581751

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 22

**Guardiola kuongeza mkataba Man City**



**Ndejembi,** Ridhiwani waanza majukumu kwa kasi

UKURASA 3



**KKKT** Dayosisi Mashariki Ziwa Victoria yapata Askofu Mpya

UKURASA 5

**THRDC** yatoa neno kuhusu mauaji albino, utekaji watoto

UKURASA 5



## RIPOTI MAALUM

# Majanga Kariakoo majengo kukosa hewa

UKURASA 4

# Kanisa la ‘Kiboko ya Wachawi’ kitanzini

• **Lapigwa** ‘stop’ huduma kuanzia leo, sababu zaanikwa... *Ukurasa 2*

## Samia asisitiza utafiti kupata majibu matatizo ya kiusalama

UKURASA 2



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akikabidhi cheti kwa mhitimu wa kozi ya 12 kwa mwaka 2023/2024, wakati wa mahafali ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) Kunduchi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **GAMONDI, NABI KUONYESHANA UBABE** UK.24 **MAONI,** UK.6

# ACT yataja mwarobaini tatizo ajira kwa vijana

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema tatizo la ajira kwa vijana kuzunguka na bahasha zenye vyeti hadi zinachakaa kwa ajili ya kusaka ajira, litamalizika iwapo serikali itaongeza nguvu zaidi katika kuwekeza kwenye kilimo na sekta binafsi ambako ndiko kuna ajira nyingi.

Kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, alisema hayo jana wakati akiwahutubia wananchi wa Manispaa ya Singida ikiwa ni siku yake ya pili ya ziara mkoani Singida katika kuhamasisha wananchi wakiunge mkono chama hicho ili kufikia lengo la kuandikisha watu milioni 10 ndani ya miezi 10 ambalo wamejiwekea.

"Wote tunajua asilimia 61 ya ajira za Watanzania zipo kwenye kilimo. Tulitegemea angalau serikali ingeona hapa ndipo mahala bora pa kuwekeza na kupata matunda haraka ya watu kuajiriwa. Leo hii kilimo chetu kimegubikwa na changamoto kibao hata bei zenyewe za mazao hazieleweki," alisema.

Semu, alisema pamoja na kwamba asilimia 25 ya kipato kinatokana na kilimo, katika hali ya kushangaza, kile kinachorudishwa ni kidogo na hii inatoa picha namna ambavyo serikali haijawekeza vya kutosha katika sekta hiyo.

"Tunashindwa kukitumia sekta ya kilimo kama eneo la kubadilisha maisha ya Watanzania ambao asilimia 61 wanategemea kilimo. Na hatuoni maofisa ugamvi, wakishughulika na kuongeza pembejeo za kilimo kwani hazitoshi. Ikumbuke, hivi karibuni kulikuwa na changamoto ya mbolea ya ruzuku ambayo ndiyo tu kwanza imeisha karibuni," alisema.

Aliongeza kwa kusema kuwa, serikali imeshindwa kuwekeza vya kutosha katika kilimo kwani asilimia 58 ya Watanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 65 wako kwenye umri wenye nguvu ya kufanya kazi lakini hakuna mazingira wezeshi ili watu wafanye kazi zitakazowapatia kipato.

"Singida, nyie mnalima alizeti leo hii bei ya alizeti haieleweki. Inabadilika, leo hivi kesho vile. Wako watu wa katikati wa kutosha alimradi mkulima anazidi kuwa mnyonge badala ya kuneemeka. Badala yake wale watu wa katikati wananufaika na kilimo," alisema.

Semu, alisema kwa kutambua tatizo la ajira nchini, ACT-Wazalendo katika sera zake itawekeza kwenye kilimo ili kuweza kupata ajira nyingi ambazo zitazalisha kazi kwa ajili ya kuwasaidia vijana nchini.

"ACT itaweka sera ya kuondoa vikwazo ili kusaidia mtu yeyote anayetaka kuanzisha kiwanda au kuanzisha shughuli ya kupata kipato ili shughuli zisizokuwa na tija ziondoke,"alisema.

Naye, Naibu Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Shangwe Ayo, aliwataka wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura na siku ya uchaguzi wawachague wagombea kutoka chama hicho ili kuleta mabadiliko.

Shangwe, alisema katika hospitali ya Mkoa wa Singida, wananchi wanalalamikia huduma mbovu za afya na kwamba hospitali hiyo haina wahudumu wa afya wa kutosha.

Naibu Katibu Mwenezi huyo aliwasisitiza wana Singida kuichagua ACT-Wazalendo kwa kuwa ni chama chenye sera bora ya hifadhi ya jamii kwa wote itayokawapa bima Watanzania wote na kutibiwa bila kujali tatizo ni kubwa kiasi gani?



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara hiyo, katika makao makuu ya wizara, eneo la Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Kanisa la 'Kiboko ya Wachawi' kitanzini

**Na Mwandishi Wetu**

KANISA la Christian Life (CLC), linaloendeshwa na Domique Dibwe, maarufu kama Kiboko ya Wachawi, lililoko Buza, Temeke mkoani Dar es Salaam, limetakiwa kufunga shughuli na huduma kabla ya leo.

Hatua hiyo ni kwa mujibu wa sehemu ya barua iliyoko mtandaoni ambayo Nipashe kupitia chanzo chake, juzi ilithibitisha kutolewa na Msajili wa Jumuiya za Kiraia, Emmanuel Kihampa, kwenda kwa kiongozi wa kanisa hilo.

Barua hiyo yenye ukurasa mmoja wa mwisho ambayo inaonyesha kutiwa saini na Kihampa, ilisambaa mtandaoni juzi na jana majira ya saa 8:00 mchana.

Gazeti hili lilipofika jana kanisani hapo, lilikuta waumini wakiendelea na ufunguaji wa vifaa, vikiwamo vipaza sauti.

Wakati vifaa hivyo vikifunguliwa, shughuli ambazo zilikuwa zikiendelea ni uuzaji wa mafuta, chumvi na maji.

Hata hivyo, baadhi ya waumini ambao hawakutaka kutoa ushirikiano kwa mwandishi wa habari hii kuhusu aliko mchungaji wao wala mawasiliano yake, walipoulizwa kinachoendelea baada ya kuwapo kwa barua hiyo, walidai wanafungua vitu hivyo kwa sababu ibada imeisha.

Katika sehemu ya barua iliyoko mtandaoni iliyoanza na kipengele b, inasomeka kuwa: "Kuweka kiwango cha fedha Sh. 500,000 kwa ajili ya kupata huduma ya maombezi, tofauti na imani ya Kikristo na kinyume cha katiba pamoja na kanuni za kanisa lako, zinazotambuliwa rasmi na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya."

Pia barua hiyo ilisema kwamba kanisa hilo linatoa mahubiri yanayodhalilisha watu madhabahuni na kutoa mahubiri chonganishi na kuhamasisha waumini kuua watu kwa dhana au tuhuma za uchawi au ushirikina.

"Kutokana na hali hiyo, kwa barua hii, unajulishwa kuwa unatakiwa kufunga mara moja shughuli na huduma zote zinazotolewa katika kanisa linaloendeshwa na Mchungaji Domique Kashoix Dibwe, maarufu kwa jina la Kiboko ya Wachawi wakati taratibu nyingine za kisheria dhidi ya kanisa la Christian Life Church zikiendelea.

"Utekelezaji wa maelekezo haya ufanyike kabla ya Julai 28, mwaka huu. Ninawatakia utekelezaji mwema wa maelekezo hayo," ilisema barua hiyo ambayo nakala yake pia imekwenda kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Pia kwa ajili ya ufuatiliaji na hatua hizo, nakala imekwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kwa taarifa na Mkuu wa Wilaya ya Temeke.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kidagaa, Shaban Ramadhan, alisema amesikia taarifa hiyo kutoka katika kijiwe cha madereva wa bodaboda maeneo hayo ambao walikuwa wakimuuliza kama amesikia kufungiwa kwa kanisa hilo.

"Baada ya taarifa hizo za kijiweni, nilipita Kiboko ya Wachawi kujiridhisha na kwa sababu utaratibu wa kiserikali unapofunga kitu kunakuwa na uzio, sikukuta uzio huo kanisani hapo.

"Nilikuta watu lakini si kama vile inavyokuaga. Wanakuwaga wengi, hivyo nimepata mashaka, ninaendelea kufuatilia zaidi," alisema.

Ramadhan alisema serikali ya mtaa wanajua mahali hapo kuna huduma ya neno la Mungu ambalo lilikuwapo hata kabla hajawa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo.

# Samia asisitiza utafiti kutatua matatizo kiusalama

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuna umuhimu wa kufanya utafiti mwingi ili kupata jawabu la changamoto za kiusalama kwa mataifa mbalimbali duniani.

Pia amesema serikali itaendelea kukiunga mkono Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) ili kiendelee kutoa michango chanya katika masuala ya kiusalama kitaifa, kikanda na kimataifa.

Aliyasema hayo jana katika mahafali ya 12 ya chuo hicho, Kunduchi, Dar es Salaam kwa wahitimu wa kozi ndefu ya mwaka 2023/24. Kati ya wahitimu 57 kutoka mataifa mbalimbali, wanawake walikuwa 12.

Rais Samia alisema serikali itakiwezesha chuo hicho kuwa kituo mahiri cha utafiti wa masuala ya ulinzi wa kimakakati ili kutatua changamoto mbalimbali zilizoko.

"Kuna umuhimu wa kufanya utafiti mwingi ili kupata jawabu la changamoto za kiusalama kwa mataifa mbalimbali duniani. Ni muhimu kuwekeza katika utafiti na kushirikiana na washirika ili kupata matokeo yanayotarajiwa," alisema.

Aidha, Rais Samia alikitaka chuo hicho kuendelea kuwekeza kimkakati kwa taifa kwa kuunga mkono utafiti zenye tija na kushirikiana na taasisi zingine za kitafiti ili kuiwezesha nchi kupata maendeleo katika nyanja mbalimbali.

Rais aliwataka wahitimu Watanzania na wa mataifa ya kigeni kutoka nchi 15 kuendeleza ushirikiano ili kuweza kupata suluhu za pamoja katika kutatua changamoto za kidunia kwa utaalam.

Kadhalika, aliutaka uongozi chuoni hapo kuhakikisha idadi ya wanawake wanaodahiliwa kusoma kozi ndefu inaongezeka.

Mkuu wa Chuo, Meja Jenerali Wilbert Ibuge, alisema wahitimu hao wamechukua mafunzo ya miezi 10 yaliyoanza Septemba, mwaka jana, na wanatarajia kuhitimu mwezi ujao.

Alisema kati wahitimu hao ni 57, kati yao 10 walikuwa wakisoma stashahada ya Mafunzo ya Usalama na Stratejia na wengine Shahada ya Uzamili.

## HABARI KITAIFA

# Ndejembi, Ridhiwani waanza majukumu kwa kasi

**Na Waandishi Wetu**

MAWAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, wameanza kwa kishindo utekelezaji wa majukumu yao mapya.

Mawaziri hao ambao ni miongoni mwa wateule walioapishwa juzi baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, walianza kutekeleza majukumu yao mara moja baada ya kutoka katika hafla ya uapisho, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Ndejembi baada ya kutoka Ikulu, alikwenda moja kwa moja katika ofisi za wizara hiyo, Dar es Salaam na kuzungumza na viongozi na watumishi huku akitoa maagizo kadhaa kuhusu utendaji kazi.

Ridhiwani kwa upande wake, baada ya kuapishwa alikwenda ofisi za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kukutana na menejimenti chini ya Mkurugenzi Mkuu, Masha Mshomba.

Hakuna kilichowekwa bayana kati ya Ridhiwani ambaye kabla ya wadhifa huo alikuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na viongozi wa mfuko huo.

Hata alipotafutwa kwa njia ya simu alisema: "Hatukuwa na mazungumzo rasmi zaidi ya kusalimiana. Nitaanza kazi rasmi Jumatatu (kesho),|" alisema Ridhiwani.

Baada ya kuwaapisha viongozi hao na wengine, Rais Samia pamoja na mambo mengine, alimwagiza Ridhiwani kusimamia mifuko ya hifadhi ya jamii isitetereke kwa kuwa inahifadhi fedha za wafanyakazi kwa ajili ya mustakabali wao baada ya kumaliza ajira.

Rais Samia alisema katika mifuko hiyo kuna miradi mingi iliyoanzishwa kwa kutumia fedha za wafanyakazi lakini haijaleta matokeo Chanya, hivyo ahakikishe kunakuwa na usimamizi makini.

Ndejembi, ambaye alikuwa akishikilia mikoba aliyopewa Ridhiwani, baada ya kufika katika ofisi za Ardhi, Dar es Salaam, alitoa maagizo mbalimbali kwa watumishi ikiwamo kuongeza uadilifu na kutenda haki katika utekelezaji wa majukumu yao sambamba na kuongeza kasi katika utendaji kazi.



Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete,

Alibainisha kuwa suala la ardhi ni gumu na linahitaji watumishi kuwa makini huku akisisitiza kuwa ni lazima watende haki huku wakizingatia sheria, kanuni na miongozo inayowaoongoza katika utendaji kazi.

Pamoja na msisitizo huo, alisema ataendeleza mazuri yote yaliyofanywa na mtangulizi wake, Jerry Silaa ambaye amekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, zikiwamo Kliniki za Ardhi ili kuleta ufanisi wa wizara.

"Sikuja kutangua torati. Yote aliyoyaanzisha mtanguluzi wangu ikiwamo kliniki za ardhi zitaendelea," alisema na kusisitiza kuimarishwa kwa mifumo ndani ya wizara ili migogoro ya ardhi isiendelee kujitokeza.

**KIKAO MTUMBA**

Jana, Ndejembi alifanya kikao na menejimenti ya wizara hiyo katika makao makuu ya wizara yaliyoko Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma na kutaka menejimenti na watumishi kuondoa urasimu na kutoa hati milki za ardhi kwa wakati.

"Tuondoe urasimu. Kama mtu ana nyaraka zote zinazohitajika, tuwape hati zao na tukumbuke sisi ni watoa huduma kwa wananchi na ni wizara wezeshi. Hati zitolewe kwa wakati na hati zilizo tayari wananchi wajulishwe waje wachukue.

Tuzidi kufanya kazi vizuri na mifumo yetu ya kiwizara kuanzia wilaya, mikoa na wizara ifanye kazi vizuri. Ni vizuri tusimamie haki ya wananchi na mifumo ifanye kazi yake kutoa haki," alisema.

**•Imeandikwa na Mwandishi Wetu na Munir Shemweta, DAR na DODOMA**


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MAALUM

# Janga Kariakoo ukosefu hewa majengo

**Na Romana Mallya**



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana



Dk. Elisha Osati

NI janga linalowanyemelea watu walioko katika maeneo yenye hali ya joto kali ambayo hairuhusu hewa ya kutosha kuingia ndani. Janga hilo linaweza kusababisha magonjwa mbalimbali yanayotokana na ukosefu wa hewa na hata vifo.

Hilo ni angalizo la mtaalamu wa afya, Dk. Elisha Osati, kwa watu hao huku wafanyabiashara eneo la Kariakoo, wanaofanya shughuli zao katika majengo yanayojengwa kwa mfumo wa ‘underground’ (msingi), kulalamikia kukumbwa na joto kali kupita kiasi.

Hayo ni maisha yao ya kila siku katika eneo hilo ambalo wengine hutumia zaidi ya saa 10 ndani ya maduka yaliyoko chini ya majengo yanayojengwa kwa mfumo huo unaolalamikiwa kwamba ujenzi wake unachangia uwapo wa joto kali kutokana na kukosekana kwa madirisha.

Osati ambaye ni Daktari wa Magonjwa ya Ndani ikiwamo moyo na mapafu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anasema athari za joto zipo nyingi. Anasema joto linapokuwa kubwa kuliko kawaida, linaweza kusababisha madhara ya kiafya na hutokea mara nyingi kwa watu wenye matatizo mengine ya afya.

“Mfano mtu mwenye matatizo kwenye moyo, kisukari au matatizo ya afya ya akili, magonjwa ya kifua, pumu na magonjwa ya kuambukiza. Joto kupindukia linasababisha mwili kupoteza maji mengi, maana yake chumvi nyingi zinabaki kwenye mwili inaweza kuleta athari kwa mwili, sehemu nyingine joto likiwa jingi sana watu huweza kufariki dunia,” anasema.

Dk. Osati ambaye ni Rais mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), anasema madhara ni makubwa kulingana na hali ya mtu, hivyo wanaokaa katika joto kali mfano wale wanaokaa chini ya majengo wanahitaji angalau kila baada ya saa moja au mbili wawe wanatoka nje kutafuta hewa safi.

Pia ameshauri watu wanaokaa katika joto kali wawe wanakunywa maji mara kwa mara hata kama hawasikii kiu na kuvaa mavazi ambayo si mazito.

Dk. Osati anasema wakishakuwa watu wazima inakuwa changamoto kubwa, madhara ya joto huwa ni makubwa kwa sababu tayari kwa umri moyo, mapafu na figo huanza kuleta shida kwa baadhi ya watu.

“Ni muhimu kujilinda kwa sababu madhara ni makubwa. Hawa watu wanaokaa huko chini wakati wote wawe na uhakika wa afya zao zikoje. Wanaweza kwenda hospitali yoyote kuangalia presha, kisukari, figo na kuangalia magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza kwa sababu kwenye joto madhara yake huongezeka sana.

“Ukiangalia Shirika la Afya Duniani (WHO) linavyosema watu wengi wamefariki dunia huko nyuma. Madhara yanayotokana na joto kali sana hasa watu wenye umri wa miaka 60 hadi 65 yameongezeka sana karibu asilimia 85 kati ya mwaka 2000 na 2004 na 2017/ 2021.

Dk. Osati anasema taarifa hizo zinaonesha wale wanaokaa kwenye joto kali wanaweza kupoteza maisha kirahisi.

**WAFANYABIASHARA**

Mfanyabiashara wa duka la nguo katika moja ya majengo yaliyoko Mtaa wa Uhuru/Congo, Kariakoo, Robert Emmanuel, anasema changamoto kubwa ya joto eneo hilo inachangiwa na utitiri wa majengo ambayo hajazingatia vigezo vya ujenzi.

“Hewa ni nzito sana hata upumuaji wa mtu unabadilika. Kiafya hii si kitu kizuri, mwili unahitaji kuingiza hewa safi na kutoa hewa chafu, kwa hali hii hewa safi unaipata wapi? Majengo hayana madirisha na Kariakoo inapokea idadi kubwa ya watu wa kila aina kila siku,” anasema.

Emmanuel anashauri wanaojenga majengo hayo kuzingatia pia, afya za watumiaji kwa sababu mwisho wa siku watajikuta wanatafuta fedha ambazo baadaye zinaishia kwenye matibabu ya afya.

Anasema wamekuwa wakifanya biashara siku saba za wiki na huzifungua kati ya saa 12 au saa moja asubuhi na kufunga kuanzia saa moja jioni.

“Kama unavyoona kwa sasa majengo mengi ya zamani yanabomolewa yanajengwa mapya tatizo ni kwamba, yanabanwa na vyumba ni vidogo sana,” anasema.

Mfanyabiashara mwingine, Alpha Mbilinyi, anasema: “Hewa tunayotegemea huku chini ni inayotokea mlango wa kuingilia ambayo ni midogo kulinganisha na idadi ya fremu. “Tunavyosema wazingatie taratibu zote za ujenzi tunamaanisha pia, hata kipindi cha mvua kutokana na ujenzi huu maji huingia kwenye baadhi ya majengo.

Nehemiah Loth, anaungana na wenzake akisema: “Athari za kiafya tunazozipata ni kutokwa jasho jingi, vipele vya joto, kizunguzungu na ni rahisi kupata magonjwa ya kuambukiza kwa njia ya hewa.

Elizabeth Mahenge, anayefanya biashara ya nguo Aggrey na Congo anasema: “Huku ni zaidi ya tanuru. Milango ya kuingia imepangwa bidhaa, korido zina bidhaa hew ani finyu. Kitendo cha kufunga duka na kupandisha zile ngazi kutoka nje mwili wote huloa. Hata fremu za juu hali ni hii.”

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, anasema kuna umuhimu wa kuwapo kwa ushirikishwaji kati yao na wamiliki wa majengo wakati wa ujenzi.

“Tunashauri ghorofa ya kwanza iwe ni maduka, ya pili kuwa kwa ajili ya machinga na ghorofa ya tatu na nne inakuwa ni kwa ajili ya kutunzia mizigo, ili kupunguza changamoto hizi na nyingine,” anasema.

Mbwana anasema idadi ya wafanyabiashara waliosajiliwa na jumuiya hiyo ni watu 6,000, wenye maduka ni kati ya 35,000 hadi 40,000. Anasema wafanyabiashara wasio rasmi kwa takwimu zao wako 6,000 lakini sokoni hapo wanakadiriwa kuwa kati ya 12,000 na 16,000.

Anasema soko hilo limekuwa likipokea watu takriban 200,000 kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili kununua bidhaa mbalimbali.

**AQRB WATOA UTAALAM**

Msanifu Majengo kutoka Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Salim Ali, anasema majengo mengi si Kariakoo tu, wanapoingia katika ujenzi mara nyingi lengo ni kumridhisha mteja.

“Kuna tofauti ya aina ya majengo na wateja, mfano mteja anapokuwa serikalini mara nyingi ni rahisi kufuata taratibu zote za ujenzi. Uzoefu wangu unaonesha majengo mengi ya serikali huwa yanafuata taratibu yanapojengwa.

“Majengo mengi ya Kariakoo ni ya watu binafsi. Kwa hiyo yapo majengo ya aina mbili, yapo ambayo yanahusisha wataalam moja kwa moja na mengine wanawashirikisha kwa muda mfupi. “Hii inasababisha majengo mengi yanapojengwa muamuzi anakuwa ni mteja mwenyewe tofauti na majengo ya serikali wanapoamua kumhusisha mtaalam, wao wapo tayari kumsikiliza mtaalam anasema nini,” anasema.

Mtaalam huyo anafafanua zaidi kwamba, wanapofanya kazi na serikali utaalam husikilizwa, lakini kwa mtu binafsi huwa ni tofauti, baadhi yao wanaweza kushauri visifuatwe.

“Kuna vile vitu ambavyo athari yake ni ya moja kwa moja kwa mwanadamu, mfano jengo ambalo halikaguliwi na mtaalam ambaye ni mhandisi wa msanifu miundo kuangalia nondo au zege. Hii ni tofauti na mtu anajenga jengo lake anakwambia sitaki dirisha na huwezi kumlazimisha, litamuathiri yeye tu kiafya.

“Athari ya namna hii haina uhusiano wa moja kwa moja, useme mimi kama mtaalam ninajiondoa kwenye ujenzi, yawezekana hataki dirisha anataka kufanya stoo huko chini,” anabainisha.

Akizungumzia kitaalam namna majengo yenye msingi (underground) yanavyopaswa kuwa, Ali anasema ni lazima kuwe na madirisha ili kuruhusu mwanga na hewa kuingia.

“Yanatakiwa kuwa na uwazi mkubwa hususan majengo mengi ya Kariakoo huweka maduka. Tunategemea kunakuwa na mpishano wa watu wengi huko chini, hivyo tunategemea kuwe na urahisi wa kufikika, yapo baadhi wanaboresha wanatumia kiyoyozi ili kuondoa mrundikano wa hewa huko chini.

“Jengo lolote huwa tunashauri kuwa na baraza zenye ukubwa wa kutosha ili kuwezesha watu kupishana kwa urahisi hata ikitokea dharura,” anasema.

Kuhusu mipangomiji, Ali anasema sheria za mipango miji hutofautiana kutoka eneo moja kwenda lingine.

Anasema sheria hizo zinaelekeza kuna eneo linapaswa kuachwa kati ya kiwanja kinapoishia na jengo linakoanzia na kiwango cha chini huwa ni mita 1.5 kwa upande wa kulia na kushoto na nyuma mita mbili na mbele mita 2.5 au mita tatu zinatofautiana kutoka eneo moja na lingine. “Kwa Kariakoo tatizo si sheria, kuna tatizo la kutekeleza sheria za mipangomiji, sheria si kwamba hazipo, zipo lakini wasimamizi ndio kuna pengo la kuzitekeleza. Ukipeleka mchoro manispaa kwa ajili ya kuomba kibali ukikosea watakurudishia mchoro urekebishe. Mimi mara kadhaa wamenirudishia huu ndio utaratibu,” anasema.

Anabaisha kwamba Kariakoo inatakiwa kuwa na maghorofa ambapo baadhi ya maeneo mwisho ni ghorofa tisa na kwingine hawatakiwi kujenga chini ya ghorofa saba.

Anasema wale wenye nyumba za chini wanapovunja hawatakiwi kujenga tena nyumba za aina hiyo bali ghorofa.

Ali anashauri katika kujenga Kariakoo kuwa ya majengo ya kisasa ni lazima kufuata sheria za mipangomiji ambazo ni nzuri, ili kuhakikisha kila kinachofanyika kinaendana na sheria zilizoko.

HABARI KITAIFA

# KKKT Victoria yapata Askofu mpya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya mashariki ya ziwa Victoria (DMVZ) imemchagua mchungaji Oscar Lema kuwa Askofu mteule wa dayosisi hiyo.

Mchungaji Lema anachukua nafasi ya Askofu Andrew Gulle ambaye aliomba kustaafu wadhifa huo. Lema anakuwa Askofu wa nne tangu kuanzishwa kwa dayosisi hiyo mwaka 1999 alitanguliwa na Manase Yona (1999- 2001), Nehemia Bomani (2001- 2007) na Askofu Gulle (2008 hadi sasa).

Askofu Mteule Lema ambaye alichaguliwa juzi katika mkutano uliofanyika jijini hapa, kabla ya kuchaguliwa, alikuwa Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo.

Katika uchaguzi huo uliofanyika wakati wa Mkutano Mkuu Maalum wa XVI wa Dayosisi hiyo ambao mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Alex Malasusa, majina manne yaliyopendekezwa na kukidhi vigezo na kupitishwa majina mawili ambayo ni Mchungaji Lema na Mchungaji Stephano Ling'hwa. Katika kura, Lema alipata kura 121 na Ling'hwa 102.

Baada ya hapo yalipendekezwa majina mengine manne yalijumuisha na walioshiriki katika kinyang'anyio cha Askofu ili kupata Msaidizi wa Askofu, hivyo Mchungaji Ling'hwa kupata kura 165 huku Mchungaji Mimi Brown akipata kura 57.

Akizungumza mara baada ya mkutano huo, Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Alex Malasusa, alisema lengo la mkutano huo ilikuwa kurejesha amani na mshikamano katika dayosisi pamoja na kufanya uchaguzi, hatua aliyosema imefanikiwa kwa asilimia 100. Alisema hivi karibuni dayosisi hiyo ilikuwa na mtikisiko ambao umelilazimu kanisa kufanya uchaguzi na kuweka viongozi wapya kwa ajili ya kurejesha umoja na mshikamano kwa waumini na viongozi. "Niwasihi viongozi wa dini pamoja na waamini wetu wote kuhakikisha matatizo yote yanayotokea kanisani yashughulikiwe kupitia sheria na katiba za kanisa kwa ujumla na si vinginevyo. Pia wanaokosea wakubali kukiri makosa yao na kuyatubu," alisema.

Kuhusu mauaji na kupotea kwa watoto, Askofu Malasusa alisema licha ya kutoa pole kwa wote waliofikwa na matukio hayo alisema hali hiyo ni ya aibu kwa taifa kuendelea kuwa na watu wanaoamini katika kufanikiwa kupitia ushirikina.

"Kama kuna watu bado wanaamini katika kushinda uchaguzi kwa kutumia viungo vya watu wenye ualibino, wanalikosea sana taifa kwani hata mataifa yaliyoendelea hayawezi kutuelewa na utandawazi huu kuendelea kuamini katika ushirikina," alisema Malasusa.

Askofu Dk. Malasusa pia aliwakumbusha wote wanye taarifa kuhusu wahusika wa vitendo hivyo, kutoa taarifa ili vikomeshwe huku akisisitiza kuwa viongozi wa dini hawatarajii matukio hayo kujirudia.

Pia aliwakumbusha waumini wa kanisa hilo kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwakani. Alisema hatua hiyo ni haki na wajibu wa kila Mtanzania.



Askofu Mteule wa KKKT Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa Victoria, Mchungaji Oscar Lema (kulia) alikabidhiwa shada la maua na Mkuu wa KKKT Askofu Alex Malasusa baada ya kuchaguliwa kuwa Askofu Mteule wa Dayosisi hiyo katika Mkutano Mkuu uliofanyika mkoani Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

Akitoa shukrani, Askofu Mteule Lema alisema anatamani kuona wanaendelea kuwa na mshikamano na kumaliza tofauti zote kuhusu yaliyopita na kuahidi kumaliza mitikisiko iliyokuwapo na kuliweka kanisa pamoja kupitia utawala bora.

# THRDC yatoa neno mauaji albino, utekaji watoto

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KUTOKANA na kukithiri kwa matukio ya kupotea na mauaji ya watu wenye ualbino nchini na utekeji wa Watoto, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), wameitaka serikali kuwajibika katika kuhakikisha wanaweka mazingira imara ya kudhibiti matukio hayo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi katika tamko lililohusisha wajumbe 55 kutoka Kanda ya Ziwa, Magharibi na Mashariki, wakiitaka serikali kupitia vyombo vyake kusimama katika misingi ya kiutendaji ili kuweka nchi salama.

Mratibu wa Mtandao huo Kanda ya Ziwa Mashariki, Sophia Donald, alisema pamoja na mambo mengine, tamko hilo linakwenda sambamba na kuitaka serikali kupitia Jeshi la Polisi na vyombo vingine kudhibiti matukio yote ya utekaji wa watoto, watu wazima, kupotea kwa watu na mauaji ya watu wenye ualbino.

"Kwa kauli ya pamoja tunakemea vitendo hivi na kuiomba serikali kuweka mkazo katika kukabiliana navyo kwani umekuwa mwendelezo kila ifikapo kipindi cha uchaguzi," alisema.

Kuhusu matukio ya utekaji na mauaji kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa na Tanzania kwa ujumla, mjumbe wa mtandao huo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza, Edwin Soko, alisema kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi kwa mwaka 2003, watoto 73 walitekwa nchini.

Alisema kati ya watoto hao, 33 walitekwa kutoka Kanda ya Ziwa na kuwa kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2024, walitekwa watu 20 wenye ualbino katika mikoa ya Kanda ya Ziwa huku mwaka huu yakitokea matukio matatu kwa mkupuo.

"Tulishuhudia Mei 4, mwaka huu, tukio la kuvamiwa na kujeruhiwa mtoto Kazungu Julius huko Geita. Mei 30, alitekwa na kuawa mtoto Asimwe huko mkoani Kagera na kifo cha Mathias Sangoma aliyekatwa mkono na kuvuja damu nyingi huko Kwimba mkoani Mwanza.

"Mwingine ni mtoto Happyness Raphael, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustiono (SAUT) Mwanza aliyevamiwa na kushambuliwa kwa mapanga na watu wasiyojulikana. Tukio lingine ni la Juni 25, mwaka huu, huko wilayani Sengerema ambako kijana Liyani Donald alivamiwa akiwa amaelala na kufanikiwa kujinasua," alisema Soko.

Mjumbe Mwingine Musa Jonas alisema matukio hayo yamekuwa yakitokea zaidi katika vipindi vya uchaguzi hali ambayo imekuwa ikijirudia mara kwa mara huku akiitaka hali hiyo iikumbushe serikali juu ya kuweka nguvu ya pamoja katika kukabiliana nayo.

Alisema kuendelea kwa matukio hayo ni ukiukwaji wa haki ya kuishi kama ilivyobainishwa katika Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 14, Mkataba wa Kimataifa wa kuhusu watu wenye ulemavu wa mwaka 2006, Tamko la Dunia juu ya haki za binadamu la mwaka 1948 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu la mwaka 1981. Kuhusu matakwa ya mtandao huo, Mjumbe wa THRDC, Sophia Nshush,i alisema wanalitata Jeshi la Polisi kuwajibika kwa kuchukua hatua juu ya matukio hayo ili kuyakomesha moja kwa moja pamoja na kutoa taarifa kwa umma mapema pindi yanapotokea katika jamii.

Pia alisema mtandao huo unamkumbusha Rais Samia Suluhu Hassan kuunda kamati huru ya kushughulikia masuala hayo kwa kuwa tangu yameanza, hakuna chombo kilichoundwa kwa ajili ya kudhibiti na kuyatolea taarifa rasmi.

"Tunaiomba serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kumaliza haraka mchakato wa upitishwaji wa rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Watu Wenye Ualibino wa mwaka 2023/24 mpaka 2027/28 ili hatua za utekelezaji zianze kuchukuliwa," alisema Nshushi. Pia alisema serikali inatakiwa kutenga bajeti maalum ili kuimarisha mifumo ya ulinzi kwa watoto na watu wenye ualibino kuanzia ngazi za vitongoji hadi taifa ili kuwa na ulinzi madhubuti.

## Mchengerwa awaonya Ma-DED kukacha vikao

**Na James Mwanamyoto,** KIBAHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameelekeza wakurugenzi wa halmashauri kuacha kuondoka katika vituo vyao vya kazi wakati wa vikao vya Kamati ya Fedha, Bajeti pamoja na vile vya Usalama ili kusimamia kikamilifu masuala muhimu ya uamuzi na kudhibiti upatikanaji wa hati chafu katika halmashauri.

Mchengerwa alitoa maelekezo hayo juzi wakati wa kikao kazi chake na wakuu wa wilaya wote nchini kilichofanyika katika Ukumbi wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha mkoani Pwani. "Inaonekana sababu kubwa ya halmashauri nyingi kupata hati chafu ni kitendo cha baadhi ya wakurugenzi kushindwa kusimamia masuala ya fedha na kutelekeza jukumu hilo kwa maofisa wa fedha na kukaimisha ofisi kila wakati, hivyo kuanzia sasa mkurugenzi yeyote asitoke kwenye kituo chake cha kazi wakati wa vikao vya masuala ya fedha," alisisitiza.

Mchengerwa aliwataka wakuu wa wilaya kutoa taarifa iwapo mkurugenzi yeyote atatoka katika kituo cha kazi wakati wa vikao vya kujadili masuala muhimu ya mipango na bajeti hasa kwenye vikao vya kamati za fedha na kamati za usalama.

"Katibu Mkuu sitegemei kusikia mkurugenzi wa halmashauri anatoka kituoni bila kumpatia taarifa mkuu wa wilaya kwani mkurugenzi anapaswa kushirikiana kiutendaji na mkuu wa wilaya. Naamini hilo halitatokea baada ya kikao hiki," alisema.

Mchengerwa pia aliwataka wakuu wa wilaya hao kuzingatia mipaka ya madaraka yao kwa kuwa wao ni kiungo muhimu cha kuimarisha ushirikiano miongoni mwa viongozi na watendaji wa taasisi zote zilizoko katika wilaya na halmashauri.

"Katika kutekeleza majukumu yenu mnapaswa kuzingatia mipaka yenu ya utendaji kazi na hatua mtakazochukua zizingatie kanuni, sheria, miongozo na taratibu zilizopo katika utumishi wa umma ili mjiepushe na ulevi wa madaraka," alisisitiza.

Mchengerwa alifanya kikao kazi cha siku mbili na wakuu wa wilaya zote nchini katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa viongozi hao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wateule wa Rais wazingatie viapo utekelezaji wajibu wao

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi aliwaapisha viongozi kadhaa aliowateua hivi karibuni kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa majukumu mapya waliyopangiwa. Viongozi hao ni mawaziri, naibu mawaziri, katibu mkuu wa wizara na makatibu tawala.

Katika hotuba yake baada ya kuwaapisha wateule hao, alitoa maelekezo kwa kila mmoja kuhusu nini anachopaswa kufanya kulingana na nafasi yake. Pamoja na maelekezo hayo, Rais aliwasisitiza viongozi hao kuwa wanapaswa kutambua kwamba nafasi za uongozi walizo nazo si za kudumu bali ni za muda huku akifananisha na koti la kuazima kuwa anayempa anaweza kumvua wakati wowote atakavyoona inafaa.

Rais pia aliwaambia viongozi hao waache kujineemesha kwa kutumia nafasi zao bali watambue kuwa wamepewa nafasi hizo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Alisisitiza kwamba hatakuwa na mswalie mtume kwa wale wote watakaoshindwa kutimiza majukumu yao kwa ufanisi na weledi huku wakifuata sheria, kanuni na taratibu.

Kubwa zaidi, aliwakumbusha kuwa hawana budi kuzingatia viapo walivyokula vya kuwa waadilifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba pamoja na kutokutoa siri za serikali isipokuwa ama katika kutekeleza majukumu yao au watakavyoagizwa na Rais.

Pia aliwasisitiza kuwa wanapaswa kuheshimu viapo hivyo kwa sababu wameapa huku wakiwa wameshika misahafu kwa mujibu wa imani zao pamoja na kile cha uadilifu chini ya Kamishna wa Sekretarieti ya maadili ya Viongozi wa umma.

Ni dhahiri kwamba kama wahenga wanenavyo lisemwalo lipo kama halipo laja, Rais amezungumza hayo kutokana na hali halisi ya wateule wengi wanavyofanya kazi zao kwa utashi binafsi badala ya kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika utendaji wao.

Baadhi ya watu wanapoteuliwa kushika nafasi fulani, hujisahau na kujifanya miungu watu, wakitaka wasujudiwe na wale wanaowaongoza huku wakitanguliza mbele maslahi binafsi ikiwamo kujilimbikizia mali, wakiendekeza ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka. Wengine wamekuwa wakifanya vitendo vya ajabu vikiwamo ukandamizaji na unyanyasaji wa kijinsia kiasi cha kuwadhalilisha waliowateua na jamii kuona kama wametumwa kufanya hivyo.

Iko mifano ya baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya ambao wamekuwa wakitumia nafasi hizo vibaya kwa kuendekeza rushwa pamoja na kuwaweka ndani baadhi ya wananchi bila sababu zisizo na msingi. Kutokana na hulka hiyo, miongoni mwa wateule hao husema moyoni kwamba wameula kwa maana ya kujinufaisha kupitia vyeo hivyo badala ya kuwatumikia wananchi.

Mbali na vitendo hivyo, baadhi ya wateule wamekuwa wakilalamikiwa kutokujali matatizo ya watu wasio na uwezo badala yake wanawakumbatia wenye fedha pamoja na kushindwa kushughulikia kero za wananchi na matokeo yake kuendelea kuwa katika matatizo na kuzidi kuwa katika lindi la umaskini.

Kauli hiyo ya Rais Samia si mara ya kwanza kusikika katika jamii ya Watanzania. Aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, pia aliwahi kusema katika miaka 10 ya uongozi wake, wateule wake wengi walishindwa kuheshimu na kuviishi viapo walivyokuwa wanakula wakati wakikabidhiwa majukumu ya uongozi.

Kwa hali hiyo, wateule wengi wamekuwa wakila viapo hivyo kwa mazoea ili kupata kile walichokuwa wakikitafuta lakini matendo yao yamekuwa tofauti na yale waliyoyatamka katika viapo vyao.

Ni wakati mwafaka sasa wateule hao wa Rais kubadilika kwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa viapo pamoja na kufuata maadili ya uogozi ambayo yameainishwa katika viapo vyao kama vile uaminifu, kutojihusisha na rushwa, kutotumia madaraka yao kwa huba na upendeleo.

Wateule hao wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia miiko iliyowekwa na kutambua kwamba uongozi ni utumishi na si kutumikiwa na pia wamepewa nafasi hizo kwa ajili ya kumsaidia Rais kutatua kero za wananchi ikiwamo kusimamia miradi ya maendeleo katika ngazi mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ufanyike mkakati kuepusha wanafunzi na kero za daladala

**MOJA** ya vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wa shule za mjini, ni kukosekana kwa usafiri wa uhakika ili wawahi shuleni kutokana na kwamba baadhi ya mabasi ya usafiri wa umma hukataa kuwachukua.

Katika mazingira hayo, baadhi yao huchelewa kufika shuleni kuwahi vipindi vya masomo au kuchelewa kurudi nyumbani na kujikuta wakikaa kwenye vituo vya daladala kwa muda mrefu.

Changamoto hiyo ipo, hasa katika jiji la Dar es Salaam ni miaka nenda rudi bila kuwapo kwa ufumbuzi wa kudumu. Hivyo, ninadhani ipo haja kwa wadau wa elimu kutafuta njia mbadala ya kuwasaidia wanafunzi.

Mwanzoni mwa miaka ya 90, kulikuwa na mradi wa mabasi ya wanafunzi, ambao hata hivyo, haukudumu kwa muda mrefu ukafa,

tangu wakati huo haujabuniwa mradi mwingine kwa ajili yao.

Ninadhani ipo haja sasa ya kuangalia uwezekano wa kubuni mradi mwingine ikiwamo na kushirikisha wazazi kuchangia fedha ili kukodisha mabasi ambayo yatakuwa yanawafuata wanafunzi.

Kwa mfano, katika shule za serikali kama za Diamond, Olimpio, Maktaba, Upanga na Zanaki, wazazi wanachangia nauli kati ya shilingi 40,000 kwa mwezi kwa ajili ya usafiri.

Hivyo, wazazi na walezi wanaweza kuangalia ni fedha kiasi gani wanawapa watoto wao kwa mwezi ili walinganishe na nauli ambayo inalipwa kupitia kukodisha mabasi.

Iwapo nauli hiyo ya shilingi 40,000 kwa mwezi itakuwa na unafuu, basi hawana kusaidia watoto wao kupitia usafiri huo hasa watoto wanaosoma mbali katika maeneo ambayo hakuna mabasi ya wa mwendo wa haraka.

Kimsingi, mabasi ya shule yanaweza kuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi, ambao huchelewa kufika shuleni au nyumbani kutokana na vikwazo vya usafiri wanavyokutana navyo vituoni.

Inasikitisha kuona wanafunzi wakiwamo wenye umri mdogo wamebeba madaftari na vitabu, wanafika kwenye vituo vya daladala, halafu wanazuiwa kupanda usafiri.

Unakuta daladala kuelekea makumbusho, Kariakoo au maeneo mengine ya jiji, kondakta anasema; "sipakii wanafunzi" kitendo kinachosabisha wengi kubaki vituoni bila usafiri.

Wakati mwingine wakipanda, wanashushwa na kuambiwa wasubiri hadi watu wazima waenee kwenye viti. Hiyo haijalishi kwamba kuna mvua au ni kiangazi, bali wanazuiwa bila kuzingatia hilo.

Hivyo, wakati wa mvua baadhi ya wanafunzi hunyeshewa, huku makondakta wakiendelea kuita abiria wengine ambao watu wazima bila huruma, waingie ndani ya daladala kwa kuwa wanaloana.

Kwa hali hiyo inavyoendelea, ni vyema kuwapo kwa hatua za kuwanusuru wanafunzi na adha hii ambayo huwa wanaipata hasa wakati wa asubuhi na jioni ikiwa ni kuwapo kwa usafiri wao.

Njia mojawapo ni kuanzisha usafiri wa mabasi ya shule ambayo ni ya kukodisha kama nilivyoeleza kuwa baadhi ya shule za serikali vina utaratibu huo unaoepusha wanafunzi kupata adha vituoni.

Bodi na kamati za shule zinaweza kuanzisha mchakato huo kwa kushirikisha na wazazi na walezi ili kuangalia uwezekano ambao utasaidia watoto wao kuondokana na mateso na kusota vituoni muda mrefu.

Kupitia vikao vya bodi na kamati hizo, ninaamini vinaweza kutoka na majibu mazuri yatakayosaidia kuwafanya wanafunzi, hasa wale watoto wadogo kufurahia elimu badala ya kuiona kama ni mateso.

Ikumbukwe kuwa, baadhi ya wanafunzi huondoka nyumbani kwao saa 11 alfajiri kwenda katika vituo vya daladala kutafuta usafiri wa kwenda shuleni, lakini hujikuta wakikaa vituoni hadi saa moja asubuhi.

Sababu kubwa ikiwa ni kukataliwa kuingia katika daladala, ingawa wapo makondakta na madereva wachache huwachukua. Lakini njia nzuri ya kuwaondoa katika kero hiyo, ni kuwapo kwa usafiri wao.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Sheria yoyote kinyume cha Katiba ni batili



Pascal Mayalla

LEO naendelea na makala elimishi za kuwafundisha Watanzania kuijua Katiba, sheria na haki. Je, wajua kuwa japo mhimili wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ndio wenye mamlaka ya kutunga sheria haliwezi kutunga sheria kinyume cha Katiba.

Pamoja na mamlaka hayo, Bunge halina mamlaka ya kutunga sheria batili au kinyume cha Katiba kwa sababu Katiba inalizuia.

Kutokana na ukweli huo, swali la kujiuliza ni kwamba je, Bunge letu limepata wapi mamlaka ya kutunga sheria batili na kwa kutumia kifungu gani?

Si tu Bunge limetunga sheria batili, bali limeuchukua ubatili huo na kuuchomekea kiubatili ndani ya Katiba yetu, hivyo kuibatilisha Katiba yetu kuwa katiba yenye ubatili!. Sasa Bunge limetunga tena sheria batili ya uchaguzi na ubatili ule ule uliokwishabatilishwa na Mahakama Kuu na kumpa Rais aitie saini ikuanze kutumika.

Kwa nini Bunge letu litutendee hivi?

Kwa kuanzia, kwanza tulijue Bunge ni nini na majukumu yake ni yapi. Ibara ya 62 (1) ya katiba inasema: "Kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge.

Bunge la JMT ni moja ya mihimili mitatu ya dola, yaani Serikali, Bunge na Mahakama. Japo mhimili wa serikali ndio unaonekana kuwa ndio kila kitu kwa sababu mkuu wa mhimili huo ni Rais wa JMT, ndie Mkuu wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, hali inayofanya serikali kuonekana kama ndio mhimili uliojichimbia chini zaidi lakini kwa mujibu wa katiba yetu na kwenye majukumu ya Bunge,

Kifungu cha pili cha ibara hiyo kinasema Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano (hivyo Bunge ni kuu kuliko serikali, kuliko mahakama) ambalo linapata ukuu wake na madaraka yake kutoka kwa wananchi na linatakiwa kufanya kazi zake kwa niaba ya wananchi.

Moja ya kazi kuu za Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote ukiwamo mhimili wa Mahakama, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii, hivyo kikatiba Bunge ndicho kila kitu,si serikali, si mahakama!.

Kifungu cha (3) kinasema Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza-

(a) Kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake;

(b) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti;

(c) Kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mfupi, muda wa kati au muda mrefu unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

(d) Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria;

(e) Kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

64.-(1) Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Bunge.

Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, ndiyo itakuwa na nguvu, na sheria hiyo nyingine, kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa batili.

Hii Ibara ya 64 (5) ndiyo inayosisitiza ukuu wa Katiba kuwa ina nguvu ya sheria kuliko chombo chochote. Katiba ina nguvu kuliko Bunge, ina nguvu kuliko serikali, ina nguvu kuliko mahakama, katiba ndiyo kila kitu.

Pia ni ibara hii, ndiyo imeipa katiba mamlaka ya juu kuliko mahakama ya kubatilisha sheria yoyote endapo itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba.

Katiba ndiyo itakuwa na nguvu na sheria hiyo nyingine kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa batili. Ibara hii maana yake ni kwamba Bunge halina mamlaka ya kutunga sheria yoyote inayokwenda kinyume cha katiba.

Hukumu ya Mahakama Kuu, katika kesi ya Mchungaji Christopher Mtikila, imezitangaza Ibara ya 39 na 63 za Katiba ya JMT ni batili, na zimechomekewa kwenye katiba kiubatili.

Mahakama Kuu umetamka kuwa katika pingamizi ya serikali kwa hukumu hiyo kwenye Mahakama ya Rufani, Hukumu ya Mahakama ya Rufani haikubatilisha hukumu ya Mahakama Kuu kuhusu ubatili wa vifungu hivyo kwenda kinyume cha katiba bali imejikita kwenye uwezo wa mahakama kuliingilia Bunge katika utungaji wa sheria.

Kwa hiyo Mahakama ya Rufani ikajitoa kuwa mahakama si "the custodian of the will of the people", "the custodian ni Bunge", hivyo ikatoa uamuzi kuwa maadam ubatili huo umefanywa na Bunge, mahakama haiwezi kuliingilia Bunge katika utungaji wa sheria, hivyo Bunge ndilo likarejeshewa kuuondoa ubatili huo.

Kitendo ilichofanya Mahakama ya Rufani hapa ni kama mtu umeibiwa gari lako, ukashtaki polisi kuwa umeibiwa, kisha ukaliona gari lako, ukaripoti polisi umemkamata mwizi wako.

Yule mwizi na ushahidi wa gari lako, akafikishwa mahakamani, mahakama ikatoa uamuzi kuwa ni kweli gari ni lako na mwizi ameliiba, na amekamatwa nalo lakini kwa vile mwizi huyu ni mtu anayeheshimika sana, mahakama imeamuru alirudishe gari alipoliiba. Yule mwizi hakulirudisha mpaka leo!

Bunge limetunga sheria batili kinyume cha katiba, mahakama ikatangaza sheria hiyo ni batili kwa sababu inakwenda kinyume na katiba.

Bunge likafanya marekebisho ya katiba kwa hati ya dharura na kuuchomekea huo ubatili ndani ya katiba kwenye Ibara ya 39 na 63 ili kuuhalalisha ubatili huo. Mahakama Kuu ikaamuru kuwa huo uchomekeaji ni batili, ibara hizo ni kinyume cha katiba.

Mahakama ya Rufani ukaliamuru Bunge, kuuondoa ubatili huo ndani ya katiba yetu na kuifuta sheria batili ile!. Kwanini mpaka leo Bunge halijatekeleza hukumu ile ya Mahakama? Na kama haitoshi, Bunge letu tukufu, likatunga sheria mpya ya uchaguzi yenye ubatili ule ule. Hii maana yake ni nini?

**Tukutane Juma lijalo.**
**Pascal Mayalla**

- **Mwandishi ni Mwanasheria na Wakili wa Kujitegemea anapatikana kwa namba 0754270403. Baruapepe pascomayalla@gmail.com**

# Tanzania mwenyeji kongamano UN utalii wa vyakula vya asili

**Na Mwandishi Wetu,**
ZIMBABWE

Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa kongamano la pili la Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani (UN Tourism), Kanda ya Afrika kuhusu utalii wa vyakula vya asili katika Bara la Afrika kwa mwaka 2025.

Katibu Mkuu wa UN Tourism, Zurab Pololikashvili, alisema hayo jana katika ufunguzi wa Kongamano la Kwanza la Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani, Kanda ya Afrika kuhusu utalii wa vyakula vya asili katika Africa linaloendelea jijini Victoria Falls, Zimbabwe.

Pololikashvili alimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, kwa ushirikiano na nia yake ya kutaka kutangaza utalii wa chakula na kusisitiza kuwa UN Tourism iko tayari kutoa ushirikiano kwa nchi za Afrika katika kutangaza utamaduni wa kiafrika hasa Utalii wa vyakula.

"Afrika si tu kwa ajili ya safari na kuangalia mazingira ya asili bali pia tunataka kuuonyesha ulimwengu kwamba ni tajiri katika utamaduni hasa utalii wa vyakula ambao ni sehemu kubwa ya utamaduni wetu," alisisitiza.

Naye Waziri Kairuki alisema kufanyika kwa kongamano hilo Tanzania kutakuwa na manufaa makubwa katika kukuza mnyororo mzima wa thamani katika utalii ikiwamo utalii wa vyakula hasa kugusa wadau wengi wakiwemo wakulima wafugaji, wavuvi,wazalishaji wa nafaka,wachakataji wa mafuta.

"Tunao mwaka mmoja wa kufanya maandalizi na tutajipanga vizuri kuhakikisha kwamba Tanzania inaonesha urithi na utajiri mkubwa tulionao lakini ni nafasi nzuri katika kukuza utalii wetu zaidi," alisema.

Waziri Kairuki alisema kupitia jukwaa hilo, kutakuwa na mashindano mbalimbali kwa ajili ya ubunifu na wenye vyuo na wataalamu wengine watapata nafasi ya kubadilishana uzoefu na wenzao kutoka nchi zingine za Afrika.

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii Tanzania (NCT), Dk. Florian Mtey, alisema kufanyika kwa kongamano hilo Tanzania kutakuwa fursa kubwa kwao kwa kuwa wamekuwa wakitoa mafunzo ya mapishi mbalimbali na kufanya matamasha ya mapishi kwa nyakati tofauti.

Kongamano hilo lilifunguliwa rasmi na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, ambaye alisisitiza umuhimu wa sekta ya kilimo katika kukuza utalii wa chakula.

# Usajili wa migogoro kwa mtandao kuleta ufanisi

**Na Halfani Chusi**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mary Maganga, amesema mfumo mpya wa kusajili migogoro ya kazi kwa njia ya mtandao, utaepusha malalamiko na ucheleweshwaji wa haki pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji wa tume.

Maganga aliyasema hayo jana jijini Dodoma, wakati akifungua mafunzo maalum ya mfumo wa kusajili migogoro ya kikazi unaofahamika kama 'Online Case Management' kwa watumishi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kutoka ofisi mbalimbali za mikoa, Tanzania Bara.

Alisema matumizi ya mifumo yanaongeza ufanisi wa utendaji kwa namna mbalimbali na pia, uwezo wa kutumika katika mazingira bila kuhitaji kwenda katika ofisi husika kupata huduma.

"Mara nyingi tukiwa tunataka kuongeza ufanisi pa kwenda ni kwenye mifumo kwa sababu unaweza kuitumia popote pale ulipo na bila kuhitaji kwenda kwa ulalisia kwa hiyo, tuna imani kubwa itakwenda kuongeza ufanisi wa tume yetu," alisema.

Aliwasisitiza watumishi kuendelea kusimamia haki katika ajira na kazi kwa kuhakikisha wanatatua migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Vilevile, aliipongeza CMA kwa kuendelea kusuluhisha migogoro ya kikazi hadi kufikia asilimia 76, akisifu ni hatua nzuri kulingana na mpango wao wa kuhakikisha wanafikia asilimia 81 kwa njia ya usuluhishi.

Mkurugenzi wa CMA, Usekelege Mpulla, alisema mfumo huu unatarajiwa kutumika kutekeleza lengo la Tume ikiwa ni kuwafikia wadau mbalimbali kwa urahisi popote walipo.

# Wapewa elimu yamatumizi ya fedha

Na Chedaiwe Msuya, MTWARA

WANANCHI kutoka maeneo mbalimbali ya Mtwara wameendelea kupata elimu ya matumizi sahihi ya fedha ambayo yameandaliwa na Wizara ya Fedha, yakihusisha wilaya zote za mkoa wa Mtwara

Katika mafunzo yaliyofanyika katika kijiji cha Nanhyanga, Wilaya ya Tandahimba, wajasiriamali na wafanyabishara walijitokeza kwa wingi kupata elimu hiyo huku wengi wao wakikiri kuwa wamejifunza mambo mengi ambayo walikuwa hawayajui kabla.

Akizungumzia programu hiyo, Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Elizabeth Mnzava, alisema wizara inafanya jambo ambalo lilihitajika kwa wananchi kwa muda mrefu huku akisisitiza kuwa sasa kutakuwa na mwamko mpya.

"Wananchi husasan wa maeneo ya vijijini wanatakiwa kuwa na uelewa wa masuala muhimu ya fedha ndiyo maana unaweza kukuta wana fedha nyingi kwa wakati mmoja na baada ya muda hawajui hata zilikwenda wapi. Kupitia elimu hii, itawakomboa," alisema Mnzava.

Naye Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Kelvin Kalengela, alisema mkoa wa Mtwara unakabiliwa na uelewa mdogo wa matumizi ya fedha kwa wananchi ndiyo maana wengi wamekuwa wakikopa mikopo inayowaumiza.

"Kuna mikopo ya aina mbalimbali inatolewa kienyeji, mingi haina sifa wala vigezo lakini wananchi hawajui ndiyo maana tunawapa elimu ili pia wasitumie fedha zao vibaya," alisema.

Habiba Shube, mkazi wa kijiji cha Tandahimba aliipongeza serikali kupitia Wizara ya Fedha na taasisi zingine zinazoshiriki katika kutoa elimu hiyo akisema itawasaidia wananchi hususan kinamama kuepuka mikopo umiza.

"Hii sisi kinamama naweza kusema inatuhusu kuliko hata wanaume. Sisi ndio wahanga (waathirika) wakubwa maana tuna shughuli nyingi ambazo zinatumia pesa, hivyo tunajikuta tunaingia kwenye mikopo isiyo na sifa tunalipa madeni, kila siku tunalipa madeni tu," alisema.

Mafunzo haya yaliyoanza mapema wiki hii, yanaendelea katika wilaya mbalimbali za Mtwara kwa lengo la kuongeza uelewa kwa wananchi juu ya masuala ya fedha kwa ujumla.

# Mafanikio Dira ya Taifa 2025 yabainishwa

Na Maulid Mmbaga

WASTANI wa umri wa kuishi kwa Mtanzania umeongezeka kutoka miaka 52 mwaka 2000 hadi kufikia miaka 66 mwaka 2022, ikiwa ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2000 -2025.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji na Mipango, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo jana jijini Arusha, lipomwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wakati akizungumzia utekelezaji na mafanikio ya dira ya maendeleo inayomalizika 2025. Katika Kongamano la Pili la Kikanda la Ukusanyaji Maoni ya Dira ya Taifa ya 2050.

Alisema lengo lilikuwa umri ufike miaka 68 ifikapo 2025 na kwenye takwimu za sasa wanawake wanaishi umri mkubwa zaidi wa miaka 68 ikilinganishwa na wanaume wanaoishi miaka 64.

"Kwa upande wa afya, mafanikio yaliyopatikana kwa miaka 25 iliyopita ni pamoja na kupungua kwa idadi ya vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua kutoka 760 hadi 104, mwaka 2000 ikilinganishwa na lengo la kufikia wakinamama 265 ifikapo 2025.

"Mafanikio mengine muhimu katika kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ni katika eneo la miundombinu ambayo ilipanuka na kuimarika. Kwa mfano, mtandao wa barabara uliongezeka kutoka kilometa 85,000 mwaka 1999 hadi 181,190 mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 113," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema mafanikio ni makubwa zaidi kwa upande vijijini ambako mtandao wa barabara uliongezeka kwa asilimia 381.4 kutoka kilometa 30,000 mwaka 2000 hadi kufikia 144,429 mwaka 2022.

Aidha, Prof. Mkumbo alisema lengo la dira ijayo ya maendeleo ya mwaka 2050 ni kuinua ustawi wa Watanzania wote kama nyenzo mama ya kuimarisha na kudumisha uhuru na furaha kwa kila Mtanzania.

Pia alisisitiza umuhimu wa kuweka mkazo na kuwekeza kwenye mageuzi mbalimbali ya kiuchumi, elimu, afya na miundombinu ili kufikia malengo tarajiwa.

"Tunapotafakari maudhui ya dira yetu ijayo ya mwaka 2025 - 2025, tuna vyanzo vikubwa vinne vya maarifa na taarifa ikiwamo kujifunza kutokana na uzoefu wetu wenyewe wa miaka 25 iliyopita na miaka zaidi ya 60 tangu nchi yetu ipate uhuru na kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na uzoefu huo, ndipo taifa litakapojua mambo gani yenye kustahili kupewa uzito katika kujipatia maendeleo lakini pia linaweza kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi zilizoendelea kwa kasi na ambazo zina mazingira ya kufanana na Tanzania.

Pia alisema baada ya kukusanya maoni ya wananchi, itaandaliwa rasimu ambayo baadae itarudishwa kwa wananchi ili kuiona na kutoa maoni yao kabla ya kuingizwa kwenye mchakato wa maamuzi ya kupitisha rasmi.

Prof. Mkumbo alisema Dira ya Taifa 2050 inaandaliwa ili iwe kionesha njia cha nchi kujua kule inakotaka kwenda na namna ya kufika. Na kwamba dira hiyo ni maono ya muda mrefu kuhusu nchi inapotaka kufika akiwasisitiza wananchi kutoa maoni juu ya Tanzania waitakayo.

"Maendeleo ni mchakato endelevu wa muda mredu, hayatokei kwa bahati, ni mipango mizuri na utekelezaji wake. Kupanga maana yake ni kuchagua. Kuchagua ni matokeo ya Kupanga na kuchagua ni matokeo ya uelewa kuwa mahitaji ni mengi lakini raslimali Nni chache," alisema. Prof. Mkumbo alisisitiza umuhimu wa kutafakari kuhusu Mtanzania wa namna gani anahitajika, jamii ya namna gani inahitajika na namna Watanzania wanavyotaka nchi yao iwe kufikia mwaka 2050.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian (wa tatu kushoto), akipokea sehemu ya msaada wa vitanda 21 na magodoro 21 kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim Tanzania, Stanley Kafu (wa nne kulia), kwa ajili ya kituo cha Afya Mwakidila, jijini Tanga mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Fredrick Sagamiko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yasisitiza mfumo thabiti takwimu

Na Mwandishi Wetu, ADDIS ABABA

TANZANIA imeushauri Umoja wa Mataifa kuanzisha mfumo thabiti wa takwimu utakaosaidia kupata taarifa sahihi kuhusu masuala ya uchumi kuelekea Azimio la Ajenda ya Hatua ya Addis Ababa.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Amina Khamis Shaaban, mjini hapa kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa kufunga kikao cha kwanza cha Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Ugharamiaji kwa Maendeleo Endelevu (FfD4) unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Alisema mfumo huo wa takwimu utasaidia kupata taarifa sahihi na kwa kuwa upatikanaji wa takwimu hizo ni muhimu hasa kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania katika kusaidia ukuaji wa uchumi jumuishi.

"Takwimu zitaongeza kwa kiasi kikubwa uwezo wa kushughulikia changamoto za maendeleo kama vile umaskini, ukosefu wa usawa, mabadiliko ya hali ya hewa, masuala ya mazingira, amani na haki," alisema.

Katika hatua nyingine Shaaban alishauri Umoja wa Mataifa kuwekeza katika mawazo ya ubunifu ili kusaidia nchi zinazoendelea katika kutumia teknolojia mpya za data, kutumia data iliyogawanywa kijinsia katika ufadhili wa maendeleo ili kutambua na kushughulikia usawa wa kijinsia.

Aliongeza kuwa ni vyema Umoja wa Mataifa itambue hitaji la njia kamili ambayo inaenea zaidi ya vipimo vya pato la taifa katika kutathmini maendeleo ya kitaifa na kutetea kupitishwa kwa viashiria vya pande nyingi.

Alisisitiza UN kutenga rasilimali kwa ajili ya ukusanyaji wa data, usambazaji, na matumizi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na ufuatiliaji mzuri wa maendeleo kuelekea Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

# MAISHA

JULAI 28, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA


Muhimu kufanya maboresho ya nyumba iliyopoteza mvuto




## UKITOKA HIVI BALAA

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | | S | H | I | M | O |
| H | | | | T | | N |
| I | | J | I | I | | G |
| M | E | I | | K | O | O |
| B | | M | I | A | | Z |
| W | | B | | | | W |
| A | P | O | N | E | | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

LAO, CHA, KOO, NOA, PENDO, AGANA, PANGA, NYOKA, CHOCHEA, ONDOSHA

## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI





## AMSHA AKILI

CHORA KWA KUUNGANISHA NAMBA KUANZIA 1-29 ILI KUPATA MCHORO KAMILI




## CHEKA



TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Roho zinazoshambulia familia nyingi

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuchambua yale yanayozisibu familia zetu. Wiki mbili mfululizo nilieleza kwa nini wanaume wengi hufa mapema tofauti na wanawake.

Nikatoa mfano wa baba mmoja aliyezungumzia yale anayoyapitia huku akihoji mbona wanaume wengi wanakufa mapema. Ni mstaafu na alieleza sintofahamu kati yake na mkewe hasa baada ya wote kustaafu.

Baba huyu akawa na hofu na mashaka kwani alichojua ni kwamba baada ya kustaafu yeye na familia yake wangeishi maisha mazuri ya mwendelezo lakini imekuwa tofauti baada ya mkewe kumbadilikia na kutomshirikisha tena yale anayofanya ikiwamo kumficha mafao yake.

Hata hivyo, nilimshauri ajitie nguvu kama baba asimame kwenye nafasi yake na amshirikishe sana Mungu kwa yote afanyayo. Mengine niliahidi kuyachambua leo ambayo ni uchawi, mizimu, misingi mibovu ya familia.

Mapenzi ya Mungu juu ya familia yalikuwa mema tangu mwanzo. Mungu alithamini na kupenda familia. Alitamani familia ziwe na upendo, ushindi na mafanikio mengi, lakini baada ya dhambi kuingia duniani hali ilibadilika.

Baada ya wanadamu wa kwanza kumwasi Mungu, laana na uovu vilianza kushambulia familia kupitia roho asi mbalimbali.

Shetani akitaka kuuangamiza ulimwengu anaanza na familia kwani anajua kuwa, akifanikiwa kuishambulia familia na kutawanya watoto tayari atakuwa ameangamiza ulimwengu.

Zipo silaha nyingi anazitumia shetani na mawakala wake kushambulia familia. Moja ya silaha ni kurusha na kupandikiza roho chafu kutoka kuzimu. Mfano wa roho hizo ni zifuatazo;-

Roho za mizimu; ifahamike kuwa, mizimu ni mapepo yanayochukua sura ya mtu katika ukoo/familia. Ni mapepo ambayo watu wa ukoo/familia waliyaita kwa hiari na kukubaliana nayo kuweka agano; na yanapata nguvu pale yanapotambikiwa.

Familia nyingi zilizotarajiwa kuwa na upendo na maisha mazuri zimejikuta zikishindwa kwa sababu ya hii mizimu. Baba niliyemjadili wiki iliyopita nilipomsikiliza na kuniambia ukoo na eneo anakotoka, niligundua kuwa ni watu wanaothamini sana matambiko.

Sasa mizimu imemsubiri amestaafu, pengine ameisahau ndipo sasa inampiga pasipo yeye kujua. Inamgombanisha na mkewe na kumjaza hofu hadi kumkosesha raha, kunakoweza kuchipua magonjwa kama presha, moyo kwenda mbio na kuishia kifo cha mapema.

> **"Zipo silaha nyingi anazitumia shetani na mawakala wake kushambulia familia. Moja ya silaha ni kurusha na kupandikiza roho chafu kutoka kuzimu. Mfano wa roho hizo ni zifuatazo;-**

Roho za mizimu zikianza kushambulia familia zinasababisha mafarakano kwenye ndoa, wanawake kuwa na roho za kiume na wanaume kuwa na roho za kike. Hivyo, zinawafanya watu wasimfuate Mungu na kuwaunganisha na roho za kiganga. Pia zinasababisha umasikini mkubwa kwenye familia.

Roho ya kichawi, hii ni silaha nyingine anayotumia shetani kuangamiza familia. Uchawi ni nguvu ya kufanya uovu na kuharibu mema. Ni roho inayoweza kupindisha hatima, kukandamiza na kutawala familia.

Uchawi umeleta uharibifu mkubwa sana kwenye ulimwengu huu tunaoishi kwani Familia nyingi zimesambaratika na hata kuangamia kwa sababu ya uchawi. Uchawi umetenganisha wanandoa, umeleta umasikini uliokithiri kwenye familia na wanafamilia kutomcha Mungu.

Roho za majini mahaba, ni mapepo mengine kutoka kuzimu yenye makao yake kwenye maji, ijapokuwa yanaweza kuishi nchi kavu. Majini mahaba yanaweza kumvamia mtu na kuanza kumshambulia, kumtawala na kummiliki.

Majini haya yameharibu familia nyingi sana kwa kusababisha mafarakano ya ndoa, mwanaume kutoka nje ya ndoa na kuzini na makahaba. Mke naye kutoka nje ya ndoa na kuzini na wanaume wengine, utasa kwa wanawake na kuua nguvu za kiume za mwanaume.

Watoto kukimbia nyumbani na kuishi mitaani na wengine kuwa wezi, kufanya ukahaba, kufeli katika elimu, kuacha kazi ghafla au kufukuzwa, kuchukiwa na familia kwa kufunikwa na giza.

Roho ya umasikini, ni roho iliyoshikilia familia nyingi na kuzifanya ziishi maisha ya mateso makubwa. Roho ya umasikini imefanya watu wengi washindwe kufurahia uwepo wao duniani.

Mtu atauliza umasikini ni nini? Ni ile hali ya kuishi katika mzunguko wa madeni. Ni kuwa na mapato yasiyokidhi mahitaji. Hapa mtu anakuwa na matumizi makubwa kuliko kipato chake.

Ni kutokuwa na uwezo wa kumiliki kitu chochote katika maisha, iwe ni nyumba, gari, ardhi. Kuishi kwa kusaidiwa na watu hata kama hutaki.

Roho nyingine ni za Mitala, ni roho ya ndoa za wake wengi, kuoa/olewa na kuachwa. Ni chanzo ndoa nyingi kuvunjika. Tuishie hapa kwa leo!

**Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Godfrey Mushi



# Ukimya ni safari ya akili kujenga misuli

RAIS Samia Suluhu Hassan anafanya usafi. Uteuzi na utenguzi wa wasaidizi wake wake inaendelea na hiyo ndiyo maana ya kufanya usafi ndani ya serikali yake.

Ni mabadiliko ya kawaida kwa mkuu wa nchi kuyafanya ili kuhakikisha serikali inawajibika vyema kwa wananchi wake.

Wiki moja iliyopita, alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri. Wako mawaziri wazoefu walioong'oka. Minong'ono imekuwa mingi lakini hakuna marefu yasiyokuwa na ncha.

Hakuna aliyezaliwa kuwa waziri. Jifunzeni kukaa kimya maana ukimya ni safari ya akili, kujikosoa.

Huko kwenye akaunti zenu za mitandao ya kijamii, andikeni hata mambo yanayohusu matendo ya huruma, badala ya kutandika mafumbo ya kifalsafa.

Mbona kutenguliwa si adhabu? Wakati mwingine kiongozi anahitaji kupanga safu anayoihitaji. Kwa mantiki hiyo, mtu anayetenguliwa ajue alikuwa katika uteuzi huo kwa hisani ya mteuzi, hivyo anapotengua pia ni uamuzi wake.

Ukimya ni safari ya akili katika kutafuta majibu. Kwa hiyo waliotenguliwa wanapaswa kujua kwamba ukimya ni safari ya akili katika kufanya vita vya kisaikolojia. Vilevile, ukimya ni safari ya akili kujenga misuli. Hapo ndipo unapojua ukimya ni safari ya akili kuingia darasani.

Jifunzeni kwamba huu ndio wakati ambao ukimya utakufanya ujue kile usichokijua. Kwamba ni wapi ulijikwaa au uliteleza na kusababisha safari yako kupata 'brake down' ya kisiasa.

Labda kuna kitu hamjakijua. Ukimya ni safari ya akili katika kuzalisha jipya. Kaa kimya, akili yako itengeneze busara maana hekima inakutaka ubakize maneno.

Rais anatekeleza vizuri falsafa yake ya 4R. Kwa hiyo, vitendo vyovyote vya kumrudisha nyuma,lazima avikemee na kulinda chama na serikali yake kwa wivu mkubwa.

Huko kwenye mitandao ya kijamii kuna mjadala mkali umeibuka baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, wengi wakihoji kilichowaondoa mawaziri Nape Nnauye (Habari, na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na January Makamba (mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki).

Katika waliotenguliwa, yuko pia Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Wadadisi wa mambo wanasema kilichofanywa na Rais Samia, ni suala la uwajibikaji. Wengine wakihusisha na kauli za hivi karibuni za mmoja wa mawaziri hao.

Licha ya Rais kutoeleza sababu za kutengua nafasi za mawaziri hao, baadhi ya watu walionyesha kufurahia kuondolewa kwa Nape, wakieleza kuchukizwa na kauli yake ya hivi karibuni kuhusu uchaguzi, waliyoitafsiri kukwaza ustawi wa demokrasia nchini.

Nape alisema kwamba matokeo ya uchaguzi hayategemei sanduku la kura bali nani anasimamamia uchaguzi, kuhesabu kura na kutangaza.

Kauli hiyo ilikosolewa na kupingwa katika majukwaa mbalimbali yakiwamo ya mitandao ya kijamii kwa tuhuma za kukiuka misingi ya demokrasia ya uchaguzi na kuheshimu uamuzi wa wapigakura.

Hata hivyo, Nape aliomba radhi kwa kauli yake hiyo huku akisema huo ulikuwa utani uliodumu kwa miaka tisa tangu atoe kauli nyingine tata kwamba chama tawala (Chama Cha Mapinduzi - CCM) kingeshinda uchaguzi wa 2015 hata kupitia bao la mkono.

Safari ya uwaziri ya Nape ilianzia mwaka 2015, alipoteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kudumu kwa muda mfupi, aliondolewa Julai 22, 2017.

Januari 8, 2022, Rais Samia alimrudisha Nape kwenye nafasi hiyo akiwa Waziri Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hadi alipomtengua.

January alipoteuliwa na Rais Jakaya Kikwete kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia mwaka 2012 na kuitumikia nafasi hiyo kwa miaka mitatu hadi 2015 alipoteuliwa na Rais Magufuli kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, kisha kumwondoa katika nafasi hiyo Julai 21, 2019.

Septemba 2021, Rais Samia alimteua kuwa Waziri wa Madini na August 30, 2023 akamhamisha kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki hadi kutenguliwa kwake. Tangu mwaka 2010, January ni Mbunge wa Bumbuli, mkoani Tanga.

Hekima inakutaka uwe na kifua cha kugandisha mambo. Hekima inakutaka uiweke nafsi yako chini ya mamlaka adilifu.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**



ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA FAMILIA YA MPONEJA BAADA YA KUMFANYIA SHEREHE YA KUMUAGA BINTI YAO SOPHIA KWA AJILI YA KUANZA MAISHA MAPYA YA NDOA. SHEREHE HIYO ILIFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NDILIMA JIJINI MWANZA HIVI KARIBUNI. PICHA: MC SARAGATA.



# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# UKITOKA HIVI BALAA



UFUMAJI wa nguo za asili kama umesahaulika, lakini ukibahatika kupata vazi la aina hiyo utafurahia kutokana na kuwa na mwonekano wa kipekee.

Nguo za kufuma kwa kutumia mitambo ya mbao inaaminika ni bora kutokana na kutengenezwa kiasili kwa kutumia mikono.

Mavazi haya yanatokana na uchakataji wa nyuzi za aina mbalimbali kama pamba, sufi, mkonge na hariri.

Aina hii ya nguo inatengenezwa na rangi ya kupendeza na kumfanya mtu kuwa na mwonekano mzuri anapovaa. Mathalani, pamba yenyewe inatumika kufuma nguo zenye rangi.


Mitindo


Kitambaa cha kufuma kinatumika katika aina mbalimbali ya mitindo ya nguo kama mashati, suruali, magauni na hata kikoi cha kuvaa kiunoni.

Hata hivyo, mtindo wa nguo inategemea mtu mwenyewe anavyohitaji. Hivyo, chaguo linakuwa la mtumiaji husika.

UREMBO

Na Mary Geofrey







# MATIBABU YA USO

UZURI wa ngozi sio rangi tu bali ni mwonekano wake kama ina afya na mng'ao unaoashiria afya njema.

Leo tushirikishane jinsi ya kufanya matibabu ya uso kwa kutumia vyakula kama kiini cha yai, machicha ya nazi, tango na limao.

Matibabu haya yanaweza kufanyika mara moja kwa wiki au kila baada ya wiki mbili, unaweza kufanya hata mara moja kwa mwezi ukipata nafasi kama unakuwa na shughuli nyingi na kupata matokeo mazuri.

Jinsi ya kufanya

Andaa maji masafi yenye joto kiasi, osha uso wako kwa hayo maji safi .

Kama una ngozi kavu au ya kati chukua kipande cha tango kidogo na upake yale maji yake usoni, kwa wenye ngozi ya mafuta unaweza kutumia kipande cha limao kwa kupaka maji yake.

Chukua pamba au kitambaa laini kwa kufuta maji ya matunda usoni kwa mtindo wa kusafisha taratibu usoni.

Chukua machicha ya nazi na sugua uso na shingoni taratibu mpaka uridhike kuwa umepata machicha.

Kisha pukuta yale machicha ubaki na uso unaong'aa bila vitu vyeupe yaani machicha.

Chukua kiini cha yai inapendeza ukitumia la kienyeji au la kisasa lenye kiini cha njano iliyokolea angalau.

Paka ule uji mzito wa njano wa kiini uso mzima bila kusahau shingoni na nyuma ya masikio na ngozi ya masikio.

Baada ya kupaka kiini cha yai unaweza kuendelea na shughuli zako huku likiendelea kukauka,linapokauka ngozi yako inakuwa kama inajivuta vuta.

Baada ya kule kuvuta kuisha inamaanisha yai limekauka kabisa. Osha uso wako kwa maji safi maji yawe ya baridi sasa.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mchuzi mzito wa nyama

WENGI tumezoea kula mboga yenye mchuzi mzito iliyoandaliwa na watu wengine kwa sababu wengi hatujui namna ya kupika.

Kwenye safu ya leo tutaelekezana namna ya kupika mchuzi mzito wa nyama ya ng'ombe.

**Mahitaji**

Nyama kilo moja, nyanya mbili kubwa, pilipili hoho kubwa moja, karoti moja kubwa,kitunguu thaumu iliyo sagwa kijiko cha chai na tangawizi iliyo sagwa kijiko cha chai.

Nyingine chumvi kiasi, kitunguu maji kimoja kikubwa na Royco pakiti moja.

**Jinsi ya kupika**

Chukua nyama yako ikatekate vipande unavyohitaji,na uioshe iwe safi kisha iweke tangawizi ambayo umesaga changanya na iweke chumvi kiasi, ibandike jikoni subiri mpaka iive vizuri na kisha ipua.

Bandika sufuria na uweke mafuta kiasi, yakipata moto weka vitunguu vyako na vikaange mpaka vibadilike rangi na halafu uweke pilipili hoho na karoti navyo vichanganye kisha chukua nyanya nazo zitie kwenye ule mchanganyiko woko, baada ya muda kidogo weka thaumu zako nazo zichanganye na mchuzi wako.

Baada ya muda kidogo weka nyama na kaanga na mchuzi wa nyanya. Subiri kwa muda kidogo kisha weka supu ambayo ulichemshia nyama na ichanganye.

Subiri hadi maji yakauke kidogo kisha weka royco na koroga vizuri hadi itakapokuwa nzito.

Hapo mchuzi wako utakuwa umeiva vizuri na tayari kwa kuliwa na chakula cha aina yoyote.



## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Muhimu kufanya maboresho ya nyumba iliyopoteza mvuto

MABORESHO ya nyumba ni jambo la muhimu yanapaswa kufanyika mara kwa mara katika kuimarisha ustawi wake.

Mbali na kufanya maboresho kwa ajili ya kuimarisha nyumba, pia huchangia kwa kiwango kikubwa iendelee kuwa na mvuto.

Msanifu majengo, Hafidhi Juma, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha zaidi na kuweka tofauti uso wa mbele wa nyumba na maeneo mengine.

"Kuna nyumba zingine zimekosa mwonekano mzuri wa mbele, hivyo kusababisha kushindwa kutofautisha uso wa mbele na wa nyuma wa nyumba au upande wa kulia na kushoto. Hapa ndipo tunasema kuna haja kwa msanifu kutumia maarifa kuandaa ramani ambayo itakidhi mahitaji ya nyumba husika," anasema Juma.

"Baadhi ya sehemu za mbele za uso wa nyumba ambazo ni muhimu kuzipendezesha ni nguzo ambayo ni sehemu ya jengo kwa kuiweka kuwa ya duara, mstatili au mraba na hii itategemea namna ilivyosanifiwa, lakini jambo la msingi ni kuhakikisha unatengenezwa kwa ustadi mkubwa," anasema.

Pia anasema katika kutengeneza uso wa mbele wa nyumba ni vizuri kutumia malighafi ambayo ni rafiki na yanavutia macho,imara na ambayo haina madhara kwa binadamu.

"Hili linawezekana kwa sababu Wasanifu wanafahamu malighafi bora za kutumia katika kutengeneza eneo hili kwa hiyo ni vema kuwatumia ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima," anabainisha.

Mbali na nguzo, mtaalamu huyo anasema madirisha nayo ni eneo muhimu ambalo linapaswa kuwekewa urembo hususani lililoko mbele ya uso wa nyumba.

"Na katika kutengeneza dirisha la mbele la uso wa nyumba, hapa napo kutategemea na vigezo vya sehemu au sababu za kisanifu, Msanifu anatakiwa kutumia utaalam wake kupendekeza aina ya dirisha kulingana na malighafi anayotaka kuweka iwe ni kwa mlalo au unyoofu," anasema

Eneo lingine la kuboresha kwenye uso wa nyumba ni anasema ni milango ya nje.

Anasema milango ya nje bila kujali aina zake, hutumiwa kwa kuzingatia aina ya mtiririko wa kisanifu ili kutokupoteza mnyororo mzima wa mtindo na mpangilio wa jengo ulivyo.

Mtaalamu huyo anashuri kwamba wakati maboresho au matengenezo yanafanywa kwa ajili ya kupendezesha uso wa mbele wa nyumba, ni vyema kutokusahau na uchaguzi wa rangi kwenye ukuta na dizaini katika valanda lake katika uso huo wa mbele wa nyumba.



## DONDOO

**Na Restuta James**



### Tumia michoro ya ramani kutengeneza bustani

UTENGENEZAJI wa bustani nyumbani au hata sehemu ya kazi unaboresha na kupendeza mazingira na hili limefanyika kwa karne zote.

Hata hivyo, ubunifu umeongeza mpangilio wa kujenga mistari ya mawe (kerbstones) na vigae vya tofali za ardhini (paving blocks), kama ardhi ngumu pamoja na upandaji miti kwa mpangilio sahihi ili kuongeza mvuto na thamani ya nyumba na mandhari yake kwa kiasi kikubwa.

Mtaalamu wa bustani, Daisy Msigwa, anasema pamoja na kwamba ukisasa umeingia kila sekta, suala la mazingira lina mchanganyiko wa ukale na ukisasa, unaotengeneza mandhari nzuri zaidi.

Anasema mandhari inayozunguka nyumba inajumuisha ardhi iliyopandwa maua, miti na nyasi kwa ajili ya kupumzika na sehemu ya paving kwa ajili ya kutembea kwa miguu au gari.


"Pamoja na maua, tunashauri na kusisitiza umuhimu wa kupanda si tu miti ya kivuli, bali ile ya matunda na eneo la mbogamboga. Eneo lenye kijani kibichi linapaswa kuwa kubwa zaidi nyumbani kwa ajili ya hewa na kupumzisha ubongo," anasema.

Anasema wako wanaopenda maji (water landscape) ambayo hujumuisha bwawa la kuogelea, la samaki, mifereji ya umwagiliaji na maji yanayoruka, akishauri watumie wataalamu hasa kwa familia zenye watoto wadogo.

"Haya yote yakiwekwa katika mpangilio sahihi kwenye eneo la kiwanja linalozunguka nyumba huongeza sana thamani ya makazi," anasema.

Anasema ili mpangilio uwe na uwiano, ni muhimu yote yakazingatia michoro ya ramani kabla ya utekelezaji. "Unapotanguliza utekelezaji bila ya michoro ya ramani ya bustani na mandhari yote ya nyumba pamoja na mahusiano yake na nyumba yenyewe, unajiandaa kukutana na tatizo kubwa hasa ubora wa kazi utakuwa wa viwango vya chini," anafafanua.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO -
SMS - 0713 447766
MWAKA HUU UTOBOI!
JUKWAANI
'TOBO GANI?"
HIVI NDUGU HELA NA UHAI WANGU BORA NINI? MAANA NAKUONA UMEKAZANIA KUNITOA ROHO!
NILIKUSIKIA UKISEMA HILI PAMBANO NIFE AU UFE WEWE! TATIZO LIKO WAPI?
ANDAMANENI KUELEKEA NILIPOSEMA ILA MSIRUDI NYUMA MIE NITAANGALIA KWENYE TIVII
WAHI KWENYE TIVII KABLA WANAO HAWAJAWAHI NAFASI KWENYE MAKOCHI
NIKIWAAMBIA KUWA KUNA MADEREVA WENGI WANAISHI DUNIANI BILA ROHO MTASEMA MANENO YA MLEVI!
USIPOTAJA VITUO MIMI SIO SHIDA ZANGU KILA ABIRIA ANAJUA ANAPOKWENDA
MWENDO WAKO WATU WOTE MAKOO YAME-KAUKA HAYATOI SAUTI!
NIPO CHINI YA MIGUU YAKO NAAPA UKIENDELEA 'KUMSOLOLEA WAIF' NAKUNYONGOLOTA SHINGO YAKO!
TOKA HUKO UVUNGUNI
HII SHUGHULI IMEFANYWA NA WAIF' JANA NIMEJISAHAU BADALA YA KURUDI NA CHIPSI, MIPOMBE IME-NIZIDI NIMERUDI NA 'GOMA!'
HII SHUGHULI AU KAKUGUSAGUSA? MWENZAKO KARUDI NA CHIPSI KAVU HAZINA TOMATO YUPO MONCHWALI
POSTI
KATA SIMU BHANA NISHAKWAMBIA LEO 'NIPO NAITI SHIFTI' NINA KAZI NZITO
MPE MPE
smoll hausi SINZA
...KINYUNYIZO CHA LEO...
"BIA TAMU KAMA UNANUNULIWA"

## HABARI KIMATAIFA

# Trump, Netanyahu wazungumzia Gaza

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amekutana na mgombea wa urais wa Marekani kupitia chama cha Republican, Donald Trump, katika jitahada za kuungwa mkono katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza.

Netanyahu, aliwasili eneo la Palm Beach, jimboni Florida, na kukutana na Trump ambaye alimwahidi endapo atachukua nafasi hiyo ataendelea kumsaidia.

Trump alisema amekuwa na uhusiano mzuri na Netanyahu licha ya kuwa na mvutano kati yao.

Hata hivyo, mgombea huyo wa chama cha Republican alitupilia mbali wazo kwamba ana mvutano kati yake na Netanyahu.

Kiongozi huyo wa Israel alimkasirisha Trump, wakati alipompongeza Joe Biden kwa kupata ushindi katika uchaguzi wa mwaka 2020.

Hivi karibuni rais huyo wa zamani wa Marekani alimkosoa waziri mkuu huyo kwa kufeli katika usalama wa Israel wakati wa shambulio la Hamas Oktoba 7, mwaka jana.

Trump pia alikosoa maoni ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, kuhusu vita katika Ukanda wa Gaza akiyaita kama ya kukosa heshima.

Benjamin Netanyahu alikutana na Harris, mgombea wa chama cha Democratic ambaye alimtaka kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano haraka.

Waziri mkuu wa Israel hapo awali alijadili makubaliano ya kusitisha mapigano ambayo yatamaliza vita katika eneo la Palestina na Rais Biden.

Kura za maoni zinabainisha kwamba Kamala Harris na Donald Trump wanakaribiana kura katika kinyang'anyiro cha kuwania Ikulu ya White House.

Benjamin Netanyahu, kwa upande wake, alitangaza kuwa safari yake nchini Marekani ingemwezesha kufikia haraka makubaliano ya kusitisha mapigano.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, alisema pande zote zinafanya kazi kufanikisha makubaliano ya usitishwaji mapigano kati ya Israel na kundi la Hamas.

Rais wa Marekani Joe Biden, juzi alizungumza na Mfalme wa Jordan, Abdullah kuhusu hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kufikiwa kwa mpango huo wa usitishaji mapigano na kuachiliwa kwa mateka wa Israel.

Hadi sasa Hamas bado inawashilia mateka 111 ambao 39 kati yao wameripotiwa kufariki katika mashambulizi ya kulipiza kisasi ya Israel.

**RFI**



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed na viongozi wengine wakiangalia eneo lililoathiriwa na maporomoko ya udongo nchini humo. **PICHA: TRT**

# Waandamanaji wadai kunyanyaswa Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

WAANDAMANAJI nchini Uganda waliokamatwa kwa kushiriki maandamano wanadai walinyanyaswa kingono wakiwa kizuizini.

Zaidi ya vijana 90 walikamatwa na wengine kushtakiwa kwa kuwa kosa la kuleta kero kwa umma kufuatia maandamano ya kupinga ufisadi yaliyofanyika katika mji wa Kampala wiki hii.

Baadhi ya wale walioachiliwa kutoka kizuizini wameripotiwa kudhulumiwa kingono na kusababisha ukosoaji. Hata hivyo, polisi walikanusha madai hayo. Maandamano ya kupinga ufisadi yalifanyika kwa siku mbili Jumanne na Alhamisi licha ya onyo kutoka kwa Rais Yoweri Museveni, kwamba waache kufanya hivyo kwa sababu wanacheza na moto.

Polisi wa kutuliza ghasia wa Uganda walivunja maandamano hayo, wakiwashika vijana kadhaa, akiwemo mtangazaji maarufu wa TV.

**BBC.**

# Senegal yawakamata wahamiaji 200

**DAKAR,** SENEGAL

JESHI la wanamaji la Senegal, limekamata mashua iliyokuwa imewabeba wahamiaji 200 katika mji wa bandari wa kaskazini wa Saint Louis.

Msemaji wa jeshi alisema watu hao kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika wamepelekwa mjini Dakar kwa ukaguzi zaidi.

Tukio hilo linajiri siku chache baada ya watu 90 kufa maji kwenye pwani ya Mauritania walipokuwa wakijaribu kuvuka eneo hilo ili kuelekea barani Ulaya.

Pia watu 25 walikufa Jumatatu katika ajali ya meli iliyotokea karibu na mji mkuu wa Mauritania Nouakchott.

Waziri Mkuu wa Senegal, Ousmane Sonko, aliwataka watu kutohatarisha maisha yao kwenye Bahari ya Atlantiki kwa kujaribu kuingia Ulaya.

Hata hivyo, njia hiyo inazidi kutumiwa na wahamiaji wengi wakati serikali ikiongeza ufuatiliaji katika Bahari ya Mediterania.

Kulingana na shirika lisilo la kiserikali la Uhispania la Caminando Fronteras, katika kipindi cha miezi mitano ya mwanzo ya mwaka huu, zaidi ya watu 5,000 wamekufa wakati wakijaribu kuwasili katika Visiwa vya Canary vya Uhispania.

**DW**

# Waliokufa kwa maporomoko Ethiopia wazidi kuongezeka

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, ametembelea eneo lililoathirika na maporomoko ya udongo na kuua watu zaidi ya 250.

Kiongozi huyo akiwa na mkewe na maofisa walitembelea eneo hilo la Kencho Shacha Gozdi, ambalo liliathirika na maporomoko hayo yaliyotokana na mvua nyingi kunyesha kwa siku kadhaa.

Hata hivyo waokoaji wanajaribu kuopoa watu waliofukiwa na udongo, lakini bado haijapatikana idadi kamili ya vifo kutokana na wengi hawajaopolewa.

Hadi sasa watu 257 wanajulikana kuwa wamekufa kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa la kutoa misaada ya kibinadamu OCHA, ambalo pia lilionya kuwa inaweza kufikia watu 500. Ethiopia iko katika hatari kubwa ya kukabiliwa na majanga ya asili yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Maofisa walisema watu wengi walifukiwa walipokimbilia kusaidia baada ya maporomoko ya awali ambayo yalifuatiwa na wengine.

Bunge la Ethiopia lilitangaza siku tatu za maombolezo kuanzia Jumamosi. Ethiopia Kusini imeathiriwa na mvua fupi za msimu kati ya Aprili na Mei ambazo zimesababisha mafuriko na kusababisha watu kukimbia makazi yao.

Taifa hilo la pili kuwa na idadi kubwa ya watu barani Afrika, mara nyingi hukumbwa na majanga yanayohusiana na hali ya hewa.

Zaidi ya watu milioni 21, wanategemea misaada ya kibinadamu kutokana na migogoro, mafuriko na ukame.

**TRT**

MAKALA

# TUBEBE DHAMANA YA WALIOTUAMINI



Na Magabilo Masambu

**Tajiri alimwita na kumwambia: "Kijana wangu kwa sasa naumwa hivyo, nakuomba kama utaweza ufanye kazi nitakulipa nitakapopona au usimame kazi kwanza kwa muda." Kijana akasema: "Hakuna shida bosi mimi nitafanya kazi utanilipa ukipona."**

ZIKO sababu nyingi zinazowafanya watu wenye nafasi wasitusaidie. Sababu kubwa ni kukosa uaminifu na kutobeba dhamana. Watu wanapothamini nafasi zetu na kutuamini kiasi cha kutupatia au kutupendekeza kupata fursa au nafasi fulani, wengi wetu hatuthamini mchango wao bali inakuwa kichocheo cha kufanya vibaya zaidi. Tunafanya kazi bila sitaha wala uadilifu kwa sababu kazi ni ya fulani tu au fulani yupo.

Kwa ujumla, tunakosa uchungu na kazi pengine tunajigamba kwa sababu aliyetupendekeza ni ndugu au jamaa yetu bila kujua pale unapoharibu anayelaumiwa ni yule aliyekuamini/aliyekupendekeza. Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana watu wenye nafasi wanaogopa kuharibu majina yao au kazi zao kwa sababu ya tabia zetu.

Mwanafalsafa mashuhuri wa Uswisi, Jean Jacques Rousseau, aliwahi kusema: "Kwa asili, watu wote huzaliwa wakiwa wema, lakini hubadilika na kuwa wabaya kulingana na matendo ya walimwengu."

Kwa hiyo ukimuona mtu hasaidii watu si kwamba alizaliwa na roho ya kutosaidia, bali ni matendo ya wanadamu yaliyomfanya awe jinsi alivyo.

Kwa ujumla, tujitahidi kuwa waaminifu pale tuaminiwapo na tukumbuke kuwa tunapoharibu tunaziba milango ya watu wengine kuwasidiwa.

Kuna hadithi ya kijana mmoja ambaye alikuwa amepigika kimaisha. Katika kusaka ugali, akakutana na tajiri mmoja kwa unyenyekevu mkubwa akaomba kazi.

Tajiri akamwamini, akamkabidhi pikipiki mpya kabisa aina ya "Boxer" na kisha akaambiwa: "Kazi yako ni kusambaza mayai kwa wateja wetu 12 na ukimaliza mapema basi siku hiyo utakuwa umemaliza kazi na nitatulipa Sh. 200,000 kwa mwezi." Kijana alifurahi mno akamiliki funguo na kuanza kazi.

Baada ya mwezi kuisha alipokea mshahara, mwezi wa pili pia. Vilevile pindi amalizapo kazi zake alikuwa anaenda kwenye shughuli zingine na pikipiki yake. Vijana waliokuwa wanamdharau wakawa hawafui dafu. Mwezi wa tatu tajiri akapatwa na maradhi na akalazwa hospitalini.

Tajiri alimwita na kumwambia: "Kijana wangu kwa sasa naumwa hivyo, nakuomba kama utaweza ufanye kazi nitakulipa nitakapopona au usimame kazi kwanza kwa muda." Kijana akasema: "Hakuna shida bosi mimi nitafanya kazi utanilipa ukipona."

Kijana aliendelea kupiga kazi, mwezi mmoja ukapita bila mshahara, mwezi wa pili, mwezi wa tatu bado tu tajiri mgonjwa. Tajiri kwa busara akamwita tena kijana na kumwambia: "Ni miezi mitatu sasa karibia wa nne hujapata mshahara wako na mimi bado mgonjwa na wiki ijayo nitarajia kwenda India kwa matibabu. Vilevile nimeamua kufunga biashara yangu, hivyo hatutaweza kuendelea na kazi. Lakini unanidai Sh. 600,000 na mbaya zaidi sina fedha mfukoni ya kutosha kukulipa.

Kwa sababu pikipiki ina miezi sita tu toka tuinunue dukani ambayo iligharimu Sh. milioni mbili, basi utaichukua ikiwa ni mshahara wako na zawadi kwako kwa kujitoa na kunitumikia."

Kijana alikubali lakini ila badala ya kufurahia, alipotoka nje aliangua kilio huku anajilaumu kwani pikipiki hiyo aliyopewa ilikuwa haitamaniki tena.

Yani alikuwa anaendesha apendavyo anabebea magunia ya kokoto, mawe na ameivunja vunja haina taa, vioo vya pembeni wala indiketa. Inawashwa kwa kuunganisha waya. Ndani ya miezi sita pikipiki ilikuwa kama ina miaka mitano

Kwa ufupi haitamaniki hata ukipewa bure huwezi kuichukua. Kijana hakuijali kwa sababu haikuwa yake. Basi kijana akabaki akisema "Ninge....."

Tunapaswa tujifunze kuwa tukiaminiwa nasi tuwe waaminifu na tukipewa kazi au chochote kile tukithamini kama chetu na tuwe na uchungu nacho. Mwandishi nguli wa vitabu wa Marekani, Mark Amend, aliwahi kusema: "Iwapo mtu yeyote amekuamini na akakubeba kwa namna yoyote, usimwangushe." Nasi tunapoaminiwa tufanye kazi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa bila kutazama ni nani aliyeko juu yetu.

Siku zote mwalimu anatamani wanafunzi wake wafaulu; Vivyo hivyo hata mtu anayekuunga mkono anatamani ufanikiwe. Iwapo utafanya kazi na ukawa unamwagiwa sifa kila mara kwa uchapakazi na uadilifu, aliyekuunga mkono atafurahi na utampa nguvu ya kuunga mkono watu wengine pia licha ya kuangalia faida kutoka kwa mtu aliyekuunga mkono.

Vilevile, unapofanya kazi kwa ubora na ustadi unajitengenezea nafasi nzuri ya kuwa na ujuzi kubwa na kupata fursa zingine kubwa zaidi. Maandiko matakatifu yanatuambia kuwa: "Ukiwa mwaminifu katika mambo madogo, utaaminiwa pia katika mambo makubwa" Wahenga nao wakagongelea msumari kwa kusema "ukibebwa bebeka usikate mbeleko."

Kwa mantiki hiyo, tuwe waaminifu na wenye kubeba dhamana ya wale waliotuamini kwa manufaa ya leo na akiba ya kesho.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania.**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Elimu ya wanamuziki wa enzi hizo kuhusu mapenzi au ndoa*



Na Adam Fungamwango

WAKATI kizazi cha sasa kinaendelea kula ngoma za mapenzi kila kukicha 'nakupenda nakupenda', kiasi kwamba wasikilizaji wake ambao ni vijana kudhani kuwa hakuna changamoto yoyote ile, hebu leo tumanikie wanamuziki wa dansi walivyokuwa wakiyazungumzia mapenzi kwa nyanja tofauti.

Mapenzi hayahaya ambayo wasanii wa sasa kila siku wanatoa nyimbo kama vile siku zote mpenzi yako poa tu, wale wa zamani walieleza changamoto nyingi kwenye ndoa na mepenzi. Kwa hiyo wasikilizaji na mashabiki wa muziki walijifunza vitu vingi kuwa ndoa ina mabonde, milima raha na uchungu wake.

Walifundishwa kuwa ndoa au mapenzi hayana raha kwa asilimia 100, bali kuna sehemu kunakuwa na changamoto ambazo wanabidi wapenzi au wanandoa kuzikabili.

Walieleza kuwa mapenzi au ndoa ni kitu muhimu kwenye jamii na kila binadamu anatakiwa kuwa nacho, lakini pia kwenye baadhi ya nyimbo wanatoa angalizo au kufundisha jinsi mapenzi au ndoa pindi zinapoingia kwenye mizozo na jinsi ya kukabliana nayo.

Kwa sasa, tumeanza kusikia watu wanauana, wanapigana, wanafanyiana mambo ya ukatili kwenye ndoa au mapenzi, nadhani kwa sababu ya kuaminishwa tu kuwa ukiingia kwenye mapenzi, basi wewe ni raha tu.

Nyimbo za kisasa zinazotolewa hata haziwakumbushi kuwa wanapoingia kwenye mapenzi au ndoa inabidi wavumiliane kwa shida na raha kwa sababu kuna mmoja anaweza kuugua, mwenzake anatakiwa kufanya kazi ya kumuuguza kwa sababu huo ndio upendo wenyewe ambao Mwenyezi Mungu anatuasa kuwa nao kupitia maandiko yake matakatifu.

Si mmoja anaumwa, mwingine anamtelekeza au kuchukua kilicho chake na kuondoka.

Kwa haya yanayotokea kwenye ndoa au mapenzi kwa sasa, hivyo wasanii wa bongo fleva sasa wana kazi ya kuelimisha ili tusisikie tena watu wakitwanga risasi, au kuuana, kufukiana shambani, kufyekana mapanga au hata kufyekana uume.

Aidha, tuangalie baadhi ya nyimbo za enzi hizo jinsi zilivyokuwa zinasawiri kuhusu mapenzi na ndoa. Tuanze na wimbo uitwao 'Ndoa ya Mateso' wa hayati Majirani Rajabu. Ni wimbo ambao mama yupo kwa mjumbe wa nyumba kumi anamuelezea matatizo ya mumewe. Anamshangaa mumewe kumtoa nyumbani kwao kwa vigelegele vingi na heshima nzuri, lakini sasa amemgeuka. Mume hashikiki, kazi yake ni ulevi na watoto hawajali. Mke anaenda kuomba ushauri kwa mjumbe.

Mjumbe anamwambia avumilie kidogo kwa sababu wameshazaa watoto. Kwa hiyo, watamwita wamkanye, akirudia basi mjumbe atakuwa shahidi kwa kitakachotokea. Na wala hatokuwa na maneno tena mke akitaka talaka yake, au kwenda kwao.

Hapa tunaona jinsi wimbo huo unavyofundisha kuwa na subira, pamoja na kwenda kuongelea matatizo sehemu husika na si kwenda kuwaambia marafiki au mashoga, ambao wengine wanakuwa ni wachonganishi tu.

Kama msikilizaji hakuelimishwa hivi, basi angeweza kusikia kaua mwenzake, au yeye mwenyewe kajiua.

Wimbo mwingine ni 'Jiko Limenuna' ni wimbo uliopigwa na Vijana Jazz, ukimzungumzia mama mmoja ambaye alikwenda kumueleza shemeji yake kuhusu matatizo yanayokea kwenye ndoa yake. Pamoja na kwamba mumewe amekuwa halali nyumbani, anacholalamika zaidi mke ni kutoachiwa hata pesa za matumizi kiasi cha kushinda na kulala na njaa.

Mke anasema angekuwa peke yake angejinyonga, lakini moyo wake wote ni kwa watoto.

Wanamuziki wanafundisha hapo kuwa hata kama mke akijinyonga kukimbia matatizo, watoto ataowaacha duniani nao wataishije? Hapa inamfikirisha hata mtu ambaye ana wazo la kufanya hivyo. Hiyo ndiyo elimu wa muziki wa zamani bwana.

Pia, wimbo mwingine ni 'Ilikuwa Lifti tu'. Ni wimbo wa Vijana Jazz, ambao mume anamtuhumu mke kuwa hamuelewi kwani amempa kijana lifti kwenye gari, lakini ni kama wanafahamiana hivi kwa tabasamu na vicheko vilivyokuwa ndani ya gari kiasi cha kumfanya achanganyikiwe.

Mke anamjibu mumewe kuwa yule ni kijana tu wa kawaida kwani alipotoka nyumbani Oysterbay kufika Selanderm gari lilizimika, yule kijana alimsaidia kusukuma na kumpa lifti tu, hivyo asiwe na wasiwasi.

Hii inaonyesha kuwa mambo haya ya wasiwasi, wivu, vingine vinavyofanana na hivyo kwenye ndoa na mapenzi vilikuwepo tangu enzi hizo na vitaendelea kuwapo. Na havikwepeki. Hebu angalia hapo, lifti tu jamaa kaanza 'kumaindi' kweli.

Vilevile, wimbo wa "Nenda Ukaishi Salama' huu ni wimbo wa UDA Jazz, unamzungumzia jamaa aliyetorokwa na mpenzi wake, akaenda kuishi na rafiki yake. Ukweli ni kwamba inauma sana. Unaweza kuua au kujiua. Lakini kwenye wimbo huu, mtunzi anamwambia mpenzi wake nenda ukaishi salama, pamoja na kuyafanya haya na rafiki yangu, lakini nakutakia maisha mema uendako.

Hapa walilenga kutuambia kwamba, chochote kitakachokupata duniani, kama hakijakuondoa uhai wako, basi maisha ni lazima yaendelee.

Unaweza kupata mume, mke au mpenzi mwingine mbele ya safari ukasahau yote na kuona kama ulichelewa, ukaanza kujilaumu kuwa hivi kwa nini nilitaka kumdhuru mtu au kujidhuru mwenyewe.

Wanamuziki na wasanii wa sasa wadhani wana wajibu wa kutunga nyimbo za kuiambia jamii yetu kuwa mapenzi si raha tu moja kwa moja hadi mwisho.

Mpenzi au ndoa yana utamu na chungu wake. Hivyo, wanapooana watafanya sherehe kubwa, lakini maisha ya ndoa yana tabu na raha zake. Aidha, uvumilivu na subira ni muhimu katika maisha ya ndoa na mahusiano, hivyo hakuna mapenzi au ndoa isiyokosa misukosuko.

Uvumilivu na subira ni alama za ushujaa katika mapenzi au ndoa kwani ngome ya mapenzi haijengwi kwa fitina, au mawimbi yanapowapiga wapenzi wakiwa kwenye safari yao

**Tuna meseji 0714 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-4

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SIKU tatu baadaye Shukuru na mpenzi wake Shani walikutana karibu na kisima cha kijiji. Hata hivyo, ilibidi waingie ndani kidogo ya pori ili wasije kuonekana na watu wengine wakiwa kwenye maongezi yao nyeti.

"Vipi kuhusu barua?" Lilikuwa swali la Shani kwenda kwa mwenzake. "Hilo ondoa shaka, ila sasa sina pesa ya kufanya sherehe." Shani alimtazama mpenzi wake, halafu akamwambia, "sawa, kuhusu sherehe na mahari nitaongea na mama ili ambebeleze baba, wewe tafuta pesa ya barua tu." "Sawa nimekuelewa." "Usiseme sawa tu nimekuelewa, fanya haraka nahisi kama kuna barua zinataka kuletwa nyumbani." "Kwa nini unahisi hivyo?" Akauliza Shukuru.


"Tayari nimeshaanza kuambiwa mambo ya kuolewa. Nimeulizwa kama atatokea mchumba nitakubali kuolewa? Nikawajibu yule ambaye nitampenda. Hapo nikaona kabisa kuna kitu." "Sawa Shani, nitawahisha barua. Ila namuhofia baba yako!" "Baba asikutie presha, najua kutakuwa na changamoto kidogo lakini mimi ndiye mtetezi wako. Mimi ndiye ninayeolewa. Mimi ndiye nitakaa na mume. Sasa haiwezekani mtu anichagulie. Nataka nikae na mwanaume ambaye moyo wangu umeridhia na siyo wa kulazimishwa." "Ambaye ni nani?" Shukuru akauliza kwa utani." "Una wazimu wewe!" Shani naye akajibu kwa utani pia. Wakagongesheana mikono kwa furaha. Wakacheka huku wakikumbatiana.

*******************************

"Mama nikwambie kitu?" "Kitu gani na wewe Shani bibiye." "Kizuri tu mama." "Haya niambie." "Nimepata mchumba." Shani alimpasha mama yake wakiwa wamekaa kwenye mkeka, wakila chakula cha usiku, huku mzee Chilambo akiwa bado hajawasili kutoka kilabuni.

Walikuwa wamekaa nje ya nyumba yao, kibatari kikiwa pembeni kikishindana na giza nene lililokuwa limetanda angani.

Kibatari kilionekana kushinda eneo dogo tu, sehemu ambayo Shani na mama yake Bi. Hanifa walikuwa wamekaa na mita chache zingine, lakini sehemu zingine kulitawaliwa na giza kwani ukipita kwenye nyumba ya mzee Chilambo, hatua kadhaa pande zote nne ukapokewa na vichaka kadhaa na nyumba nyembamba iliyokuwa na majani marefu pembeni kabla ya kukutana na nyumba zingine za kijiji hicho.




**"Mama mimi mwenyewe ndiyo nimeamua, kama ni kuishi pangoni, kulala na njaa, kufanya nini mimi niko tayari na wala siwezi tena kuja kwenu kwa ajili ya kufuata mahitaji bali nitakuja kuwasalimia tu."**

Nyumba nyingi kijijini hapo zilikuwa hivyo, mtu mmoja alikijenga nyumba yake na wa pili anakuwa mbali na eneo lote hilo linakuwa linakuwa linamilikiwa na mtu mmoja mpaka ukapokutana na mtu mwingine baada ya safari ya kama dakika 10 hivi. "He!" Mama Shani akashangaa, akamtazama binti yake, halafu akamuuliza "Haya niambie ni nani." Shani aliiangalia pembeni kukwepesha macho na mama yake, halafu akatazama chini kwa aibu. Hakujibu chochote "Niambie basi mama, ongea mtoto mzuri." Mama akambembeleza binti yake. Shani akarudisha tena macho kwa mama yake kisha akakwepesha kwa upesi huku akitazama pembeni, bado alionekana aibu imemshika. "Sasa kama huniambia mimi mama yako utamwambia nani?" Bi. hanifa aliongea kwa sauti ya upole. Shani akarudisha macho kwa mama yake, na akaongea kwa kumnong'oneza, "Shukuru." "Nani?" Mama akauliza kama vile hajasikia na binti akamwambia tena, "Shukuru." Ingawa alijitahidi sana kuficha mshtuko mbele ya binti yake, lakini Shani aliuona mshtuko huo kwa mama yake. "Mama huyo ndiyo niliyetokea kumpenda na nilikwambia tangu mapema kuwa nitakubali kuolewa kwa mtu ambaye nitamchagua mimi mwenyewe. Sasa ndiye niliyemchagua na niko tayari kuolewa naye hata leo hii." "Lakini mwanangu, huo ni uchaguzi sahihi kweli kwako?" "Kwa nini?" Shani aliuliza, Mmmh! Kijana yule hohehahe, hana kitu atakupa nini? Hana kazi wala bazi, anaweza kukutunza kweli. Isije ukawa umeolewa lakini sisi ndio tunaendelea kukulisha na kukutunza, tena ukatupa kazi ya kumlisha na mwenzako."

"Mama mimi mwenyewe ndiyo nimeamua, kama ni kuishi pangoni, kulala na njaa, kufanya nini mimi niko tayari na wala siwezi tena kuja kwenu kwa ajili ya kufuata mahitaji bali nitakuja kuwasalimia tu."

"Basi mama nimekuelewa, subiri baba yako akija nimwambie ili tujue tunaanzia wapi? Na tunaishia wapi?"

"Nakuamini mama, usiniangushe, maana baba haeleweki yule." Wakaangua kicheko huku akimalizia kula wali maharage na kachumbari iliyochanganywa na siki.

*******************************

Wiki moja baadaye nyumbani kwa mzee Chilambo zililetwa posa mbili, zilipishana kwa siku tatu. Ya kwanza ilikuwa ni ya Shukuru, lakini baada ya siku tatu kupita walipokea wageni wengine kutoka kijiji cha jirani, Mtapenda.

Zote zilifanyiwa kazi, barua za uchumba mbili, mchumbiwa ni mmoja, hivyo lazima moja ipigwe chini. Je ya nani itakataliwa? Mathalani, katika upembuzi wa kina uliofanywa na wazazi wake, ambapo ulilenga barua moja ikataliwa na nyingine ikubaliwe.

Iliyokubaliwa ni ya Fotu, kijana kutoka kijiji cha jirani Mtapenda, huku ya Shukuru kutoka kwenye kijiji hichohicho Lalanguru ilionekana kukosa sifa.

Wakati hilo linafanyika, Shani aliambiwa akaishi kwa shangazi yake kwa muda wa wiki mbili wakati wazazi na watu wa karibu wanajadili posa zilizoletwa. Hivyo, hakujua chochote kinachoendelea. Bi. Hanifa alikuwa mmoja wa waliofahamu kila kitu kwani alikuwapo hapo nyumbani, ingawa hakushirikishwa kwa asilimia 100, hasa maamuzi ya mwisho wa vigezo vya kumpitisha kijana atakayekuwa mchumba wa Shani, hivyo Mama Shani alikereka sana.

Wakiwa amekaa ndani ya nyumba yao, usiku muda mfupi tu kabla ya kulala, akatoa dukuduku lake. "Hivi mume wangu, kwa nini umeikataa barua ya posa ya Shukuru?" Mzee Chilambo akamtazama mkewe, halafu akamuuliza, "kwani wewe ndiyo unataka kuolewa?"

"Hayo sasa matusi baba Shani, yaani mimi ndiyo nataka kuolewa kweli? Hujanitendea haki, mimi nimeuliza kwa heri tu." "Haya ngoja nikujibu vizuri, kwa sababu ilikuwa ni lazima moja ikataliwe!" Akajibu kwa sauti kubwa iliyomkera mkewe. "Kwa nini mmechukua maamuzi ya mwisho bila hata kuniuliza kwa sababu mimi ndiye ninayeshinda na binti yetu. Yeye anaona nini? Na anataka nini? Hivi unajua yeye nani anamtaka kati ya hawa wawili?" Akahoji Bi. Hanifa. "Mimi ni mwanaume na ndiyo baba wa humu ndani, nina maamuzi yangu, tena ndiyo ya mwisho. Nimeamua kuwa simtaki Shukuru. Haiwezekani, mimi ni fukara, halafu binti yangu aolewe na mtu lofa kabisa yaani, hata mimi ninauafadhali." "Kwa nini tusimpe uhuru binti yetu achague mchumba anayemtaka?" "Sikiliza mama Shani, isije baadaye sisi ndiyo tukabeba mzigo wa kulea familia, yaani binti ameolewa, badala ya kukaa kwa mumewe akae hapa na mumewe, na watoto tufanye kazi ya kuwatunza sisi, hilo hapana kwa kweli mke wangu.

Mimi nimeona mbali, mpaka nikaamua kumchagua kijana kutoka kijiji cha Mtapenda ndiye amuoe binti yetu, mimi na tuliokaa tumefanya upembuzi yakinifu kabisa."

"Kwa nini maamuzi ya Shani yasiheshimiwe?" "Hayawezi kuheshimiwa kwa sababu hana akili kwani amempenda mtu ambaye hana kitu ili yeye mwenyewe apate shida na watoto wake, hivyo asituletee shida na aibu sisi hapa nyumbani." Mzee Chilambo alinena kwa msisitizo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# MWAITEGE: 'MIMI NI MZIMA WA AFYA'



MWIMBAJI wa muziki wa Injili, Bonny Mwaitege amejitokeza hadharani na kueleza yeye ni mzima na kwamba hajafariki.

Kupitia mtandao wa kijamii, Mwaitege amesema kukaa kwake kimya hakutokani na ugonjwa wala kupata ajali, hivyo akawataka mashabiki zake kupuuza taarifa hiyo.

"Nilitaka kujitokeza hadharani nizungumzie habari hizo za uwongo. Niliwahi 'kuuawa' kwenye mitandao ya kijamii mara kadhaa, lakini safari hii ilinishtua sana. Kwa kawaida huwa napuuza lakini kwa hili nilitaka kuja kusafisha hali ya hewa, mimi sijafa ni mzima." Amesema kupitia video fupi.

## ACHENI KUMSAKAMA MZEE WA TIKTOK



MWANAMUZIKI mkongwe wa taarabu aliyepata umaarufu mitandaoni, Seif Kisauji, maarufu kama Babu wa Tik Tok, amesema anaendelea kula bata hata kama kuna baadhi ya watu hawampendi.

Amesema licha ya kupata matatizo mengi kutokana na umaarufu wake, bado anaendelea kupata mafanikio kupitia mtandao wa Tik Tok, ikiwamo kununua gari jipya analotamba nalo mitaani.

"Waache watu wanitukane, lakini mimi naendelea kutamba na kula bata ninavyopenda. Nashukuru familia yangu kwa sasa inaniunga mkono kwa kila kitu ninachokifanya hivyo sina tabu," amesema Babu wa Tik Tok.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**WILLIAMS SAFI BARCELONA**
KLABU ya Barcelona imefikia makubaliano ya kumsajili winga wa klabu ya Athletic Bilbao na timu ya taifa ya Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, kwa mkataba wa miaka mitano, ambao pia utakuwa na kipengele cha nyongeza ya mwaka mmoja. **(Nicolo Schira)**

**RABIOT NA MAN UNITED**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini Manchester United baada ya kuondoka Juventus mwishoni mwa mkataba wake. (**Mail**)

**SETFORD ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL inajiandaa kumsajili mlinda mlango wa Uingereza, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ajax kabla ya ziara yao ya kwenda Marekani. **(Evening Standard)**

**LINDSTROM KWA MKOPO EVERTON**
KIUNGO wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kucheza kwa mkopo wa msimu mzima pale Everton kutoka Napoli. (**CalcioMercato**)

**GOMEZ AWINDWA BRIGHTON**
KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez mwenye umri wa miaka 21.**(Sky Sports)**



**HARRIS AWANIWA BIRMINGHAM**
KLABU ya Birmingham City imeelekeza macho yao kwa kiungo wa Fulham na Wales, Luke Harris mwenye umri wa miaka 19. **(Football Insider)**

**ARSENAL YAKOMAA NA CALAFIORI**
ARSENAL imeongeza juhudi zao za kumsajili beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, kutoka Bologna. (**The Athletic**)

**N'GOLO KANTE KUTUA WEST HAM**
KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 33 kutoka Al Ittihad. **(The Athletic)**

**ASTON VILLA KUMPIGA BEI DIGNE**
ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 31. (**Football Insider**)

**UGARTE ANUKIA MAN UNITED**
KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na Paris St-Germain. (**Fabrizio Romano)**

**MCTOMINAY AWEKEWA BEI**
MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. (**Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




**MANCHESTER,** England

## Yatoa thamani ya nyota huyo huku klabu za Barcelona na Real Madrid zikitajwa ku....

KLABU yoyote inayotaka kumsajili fowadi wa Manchester City, Julian Alvarez wakati wa dirisha la usajili la majira haya ya joto italazimika kukubaliana na kifurushi chenye thamani ya angalau pauni milioni 75 kwa mujibu wa ripoti.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina hakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara msimu uliopita akiwa amefunga mabao 11 na asisti tisa.**

Alvarez alianza michezo 31 ya ligi wakati wa msimu wa 2023/24 lakini anafikiriwa kutamani kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza.

Chaguo lake la kwanza linaripotiwa kuwa Real Madrid, wakati Rais wa Barcelona, Joan Laporta anataka kumsajili fowadi huyo pamoja na mwenzake Erling Haaland kama sehemu ya kampeni zake za kuchaguliwa tena.

Hata hivyo, The Athletic imedai City haitamruhusu kuondoka kwa bei nafuu.

Mabingwa hao wa England wanataka takriban pauni milioni 60 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anawiwa na Atletico Madrid.

Kikosi cha Diego Simeone hakiko tayari kuvuka umbali huo ili kumnasa Alvarez, wakati Paris Saint-Germain na Chelsea pia zimetajwa kumuwania.

Rais wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo tayari amekiri kuwa hatarajii City kumruhusu mshindi huyo wa Kombe la Dunia kuondoka msimu huu wa majira ya joto.


City tayari wana wasiwasi juu ya mustakabali wa mlinda mlango Ederson, huku Guardiola hivi majuzi akikiri kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anatathmini chaguo lake msimu huu wa majira ya joto.

Hata hivyo, kocha huyo wa zamani wa Barcelona alikanusha zaidi alipotangaza kiungo mahiri Kevin De Bruyne hataondoka Etihad msimu huu.

Kwa upande wa uhamisho unaokuja, City tayari wametangaza usajili wao wa kwanza kwenye dirisha hili kwa winga Savinho, 20, ambaye msimu uliopita alicheza kwa mkopo Girona kutoka Troyes.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA KUONGEZA MKATABA MAN CITY



**LOS ANGELES,** Marekani

PEP Guardiola amesema hajakataa kusaini mkataba mwingine wa kuendelea kubakia kwenye klabu ya Manchester City.

Guardiola alipendekeza mwishoni mwa msimu uliopita kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa mkataba wa sasa ambao unamalizika 2025.

Lakini akizungumza kwenye ziara ya klabu hiyo ya kujiandaa na msimu mpya Marekani, kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 alisisitiza bado anaweza kuamua kusalia klabuni hapo.

"Najua labda sikuwa sahihi kusema wakati tuliposhinda Ligi Kuu, lakini nasema kwamba nimekuwa Man City kwa miaka nane," alisema Guardiola.

"Ndio maana nakaribia kuondoka kuliko kukaa. Lakini sijasema naondoka.

"Nikitoka nitasema naondoka lakini sijasema.

"Sitakataa kabisa kuongeza mkataba. Nataka tu kuwa na uhakika ni uamuzi sahihi, sio kwangu tu, kwa klabu pia."

Guardiola anajiandaa kwa msimu wake wa tisa kama kocha wa City, amekuwa hapo baada ya miaka minne Barcelona na mitatu akiinoa Bayern Munich.

Amepata mafanikio ambayo hayajawahi kushuhudiwa tangu alipowasili mwaka 2016, akishinda mataji sita ya Ligi Kuu ya England na Ligi ya mabingwa Ulaya.

Nyongeza ya mwisho ya mkataba ilikubaliwa Novemba 2022 na alikuwa anatarajiwa kutafuta kazi ya timu ya taifa mwishoni mwa mkataba wake mnamo 2025.

"Sijazingatia kwa sababu sijaamua kuondoka," aliongeza Guardiola.

"Nikiamua, sawa yamekwisha, kwanza kabisa, nitazungumza na Mkurugenzi wangu wa michezo, Mwenyekiti wangu, Mkurugenzi Mtendaji wangu. Hiyo ndiyo ya kwanza.

"Sitawahi kufanya hatua moja bila timu yangu, klabu yangu kutojua. Ninashukuru sana. Ikitokea tutazungumza. Lini? Sijui ni lini bora zaidi.

"Haimaanishi kuifanya kwa njia hiyo ni kamili, au kuifanya kwa njia nyingine ni kamili. Au labda katika miezi michache, nitasema, kuongeza mkataba. Kwa hivyo sijui."

# Barcelona yawekewa ngumu kwa Olmo

**BARCELONA,** Hispania

RB Leipzig imekataa ombi la Barcelona ambalo linafikia punguzo la thamani ya euro milioni kwa mshindi wa Euro 2024, Dani Olmo, ripoti nchini Ujerumani zinasema.

Baada ya kuumia kwa Pedri katika robo fainali, Olmo alionekana kuwa mtu muhimu kwa Hispania katika ushindi wao wa Euro 2024 mapema msimu wa joto.

Kiungo huyo mshambuliaji alipachika mabao matatu na kutoa pasi mbili za mabao kwa taifa lake, likiwemo la ushindi katika pambano la nusu fainali dhidi ya Ufaransa mjini Munich.

Olmo amekuwa akihusishwa sana na kutaka kuondoka katika klabu yake ya sasa ya RB Leipzig, huku Barcelona, Manchester City, Manchester United na Bayern Munich zikiwa na nia ya kutaka huduma yake.

Wawaniaji wa Olmo, wamekosa dirisha lao la kuanzisha kifungu cha kutolewa cha euro milioni 60 kilichopo kwenye mkataba wake na RB Leipzig.

90min ilifichua mwanzoni mwa Julai kwamba Barcelona walikuwa wametoa ofa ya mdomo kwa Olmo, ambaye wanaamini anataka kujiunga nao zaidi ya wahusika wengine wanaovutiwa, na Sky Germany iliripoti kwamba ofa imekataliwa na Leipzig.

Ofa hiyo hiyo inaelezwa kuwa 'ilikuwa chini ya matarajio ya Leizpig', huku vyombo vya habari vya Hispania vikipendekeza ofa hiyo iwe ya euro milioni 40 ya malipo ya uhakika pamoja na nyongeza zinazoweza kuhusishwa na utendaji zinazofikia hadi euro milioni 20.

Hata hivyo, euro milioni 40 za awali zingepokelewa tu kwa awamu zilizolipwa kuanzia Januari 2025, ikimaanisha kwamba Leizpig haitapokea fidia wakati wa miezi sita ya kwanza ya mchezaji huyo huko Katalunya.

# Ten Hag ataka kikosi kipana Man United

**LOS ANGELES,** Marekani

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema anataka kuongeza upana wa kikosi chake kabla ya msimu mpya kuanza.


United imewasajili Leny Yoro na Joshua Zirkzee kuchukua nafasi ya Raphaël Varane na Anthony Martial walioachwa.

Na ingawa Ten Hag alikataa kuweka namba kwa wachezaji wapya ambao angependa kuwasajili kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili, alikiri klabu hiyo inaangalia nyota wapya.

"Tunahitaji kikosi kiwe na nguvu iwezekanavyo," alisema Ten Hag katika mkutano na waandishi wa habari.

"Tayari tulikuwa na manunuzi mawili mazuri sana, hivyo kila mtu anapokuwa fiti tunakuwa na timu ambayo inaweza kumshinda kila mtu, lakini kwa kina kikosi lazima tufuate kwa sababu tulikuwa na majeruhi, tuko hatarini.

"Lazima tuepuke hili kwa kupata majeruhi kidogo na pili, kikosi chetu kinapaswa kuwa kizuri. Ubora tulionao kwa kina ni lazima tuukamate, lakini zaidi kwa sababu msimu huu utakuwa ni uhai wa walio fiti zaidi."



Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United inaangazia mabeki wa kati, viungo wa kati na mabeki wa pembeni.

Beki ya kushoto ipo kwenye wasiwasi huku Tyrell Malacia akiwa bado hajawa fiti baada ya kukaa nje ya uwanja kwa mwaka mmoja huku kukiwa na mashaka juu ya mustakabali wa kiungo Casemiro.

"Tunaangalia katika nafasi zote ili kuongeza nguvu na tunatafuta mpango katika kikosi chetu ili kujihakikishia kuwa tuko kila wakati," alisema Ten Hag.

"Tunafanya kazi mara kwa mara na jambo zuri ni kwamba tayari tumesajili wachezaji wawili na ni mali ya klabu kama Man United ambayo unatafuta nafasi ambazo ni bora zaidi na bado tuna muda hadi tarehe ya mwisho Agosti 30.

"Mzigo na shinikizo kwa wachezaji ni kubwa, kwa mtindo mpya huko Ulaya. Niliitaja hivi punde, ni kunusurika kwa kiwango bora."

Ten Hag anaongoza ziara yake ya tatu ya kujiandaa na msimu mpya kama kocha wa United chini ya umiliki wa Sir Jim Ratcliffe.

Alilazimika kuvumilia hali ya wasiwasi kwa wiki tatu kufuatia Kombe la FA kabla ya kujua kwamba angesalia, lakini Ten Hag amesisitiza kuwa ni wakati wa kusonga mbele baada ya kutokuwa na uhakika.

"Sasa tuko katika msimu mpya, tumeacha kila kitu nyuma, tunatazamia, ni mradi mzuri," alisema Ten Hag.

"Mchakato ni mzuri, tunaenda na kupanda na kushuka na sasa tuna nguvu nyingi, nguvu nzuri, roho nzuri, tunatazamia, tunataka kufanya kazi na tunataka kushinda.

"Sidhani kama niko katika nafasi nzuri au dhaifu, nataka kushirikiana. Siwezi kufanya hivi peke yangu, wachezaji, wafanyikazi, uongozi, kila mtu. Nina hakika tutapata mafanikio zaidi. "

Licha ya kusaini mkataba mpya, Ten Hag aliiambia ESPN kwamba anafahamu kikamilifu matarajio ya mafanikio katika klabu hiyo.

HABARI MICHEZO

# SIMBA SC, COASTAL WAKUTANA KUJADILI SAKATA LA LAMECK LAWI

**Na Shufaa Lyimo**

VIONGOZI wa Klabu ya Simba na Coastal Union wamekutana jana mchana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuzungumza kuhusu sakata la usajili la mchezaji Lameck Lawi ili kufikia makubaliano kama walivyoagizwa na Kamati ya Hadhi na Sheria ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Agizo la kikao hicho lilitolewa na kamati hiyo kupitia kikao chake kilichofanywa siku kadhaa nyuma kufuatia mvutano wa usajili wa beki huyo.

Ikumbukwe Simba ilitangaza kumsajili beki huyo na kulipa fedha za usajili kwa Coastal Union lakini uongozi wa klabu hiyo ya Tanga ulikanusha taarifa hiyo na kudai Simba walivunja makubaliano yao ya awali ya usajili wa nyota huyo na kuleta mvutano kabla ya sakata hilo kupelekwa TFF.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Coastal Union, Steven Mguto, alisema baada ya kikao hicho majibu yatarudishwa katika kamati hiyo ili iweze kutoa maamuzi yake.

"Leo (jana) Simba na Coastal wanakutana mchana huu kuzungumzia suala la Lameck Lawi watakayokubaliana watayapeleka kwenye kamati ili itoe maamuzi yake," alisema Mguto.

Alisema kwa kuwa kikao hicho kinafanyika kwa maagizo ya kamati ya TFF, wao (kamati hiyo) ndio watakaozungumza kutokana na kile klabu hizo watakachokuwa wamekubaliana.

Katika hatua nyingine, Mguto alisema timu yao kwa sasa inaendelea na kambi ya mazoezi Visiwani Zanzibar kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 8 mwaka huu dhidi ya Azam FC.

Alisema malengo yao ni kufanya vizuri kwenye mchezo huo ambao ni maalum kwa ajili ya ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu itakayoanza Agosti 16.

"Malengo yetu ni kufanya vizuri katika michezo yetu yote tukianzia na ile ya tarehe nane kwani kikosi tulichonacho tuna imani tutafanya vema," alisema Mwenyekiti huyo.

## Gamondi, Nabi kuonyeshana ubabe leo

INATOKA UK. 24

ua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza tangu 1998, na kuipeleka moja kwa moja mpaka robo fainali, ikiweka rekodi ya kufika kwa mara ya kwanza tangu mfumo huo uanzishwe 1997.

Akizungumzia mchezo wa leo, Gamondi alisema haangalii sana matokeo ya ushindi bali kutazama wachezaji wake wanafanya nini uwanjani kwa kile alichowaelekeza pamoja na kujaribu mifumo mbalimbali watakayoitumia msimu huu.

"Tunafuraha kuwa hapa, tupo na wenzetu Kaizer Chiefs kwa ajili ya mechi za kirafiki za kimataifa za 'Pre season', kwanza tunawashukuru mashabiki wa timu hii kwa kutupa sapoti na kutushangilia katika mechi yetu ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Tunakwenda kucheza mechi ya kirafiki, ni mchezo ambao tutautumia kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao, tunaenda kuonyesha burudani, soka safi, tunachezesha wachezaji tofauti tofauti, siangalii sana matokeo, bali timu inachezaje," alisema Gamondi.

Mara ya mwsiho timu hizo zilikutana mwaka jana, Julai 22, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, katika mechi ya tamasha la 'Wiki ya Mwananchi', Yanga ikishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Kennedy Musonda.

Mechi ya leo itakuwa ya tatu kwa Yanga tangu ifike Afrika Kusini, ambapo ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya FC Augsburg ya Ujerumani JUlai 21 kabla ya kushinda kwa bao 1-0 katika mchezo wa pili dhidi ya wenyeji TS Galaxy, Jumatano iliyopita.



KIKAPU



Mchezaji wa timu ya mpira wa Kikapu ya Vijana, Evaresti Matiko, akijaribu kufunga goli huku akizongwa na wachezaji wenzake kwenye mazoezi ya timu hiyo katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Karihe aahidi mabao mengi Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI mpya wa klabu ya Mashujaa FC, Seif Karihe, amesema atahakikisha anapambana kuipatia timu yake mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine ili ifanye vizuri msimu unaotaraji kuanza hivi karibuni.

Karihe, alisema amefurahi kujiunga na klabu hiyo yenye mashabiki wanaoipenda timu yao na kwa kushika nafasi ya tatu ya timu zilizoingiza watazamaji wengi msimu uliopita.

Akizungumza akiwa kambini kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao, Karihe aliyejiunga akitokea Mtibwa Sugar iliyoshuka daraja, alisema anaamini bado atakuwa na uwezo uleule wa kufunga mabao na kwa sababu amekutana na wachezaji bora kwenye kikosi hicho.

"Mimi ni mshambuliaji, kazi yangu kubwa ni kufunga, na kila ninapokwenda huwa naacha alama, hata Mtibwa Sugar pamoja na kwamba imeshuka daraja lakini nilifunga mabao mengi, nimejiunga hapa na kukuta hali ya kambi ni nzuri, ushirikiano na wachezaji wenzangu uko vizuri hiyo imenifanya nizoee mazingira kwa haraka, tuseme ukweli tu kuwa hakuna ugeni kwenye mpira, wachezaji mkishakutana hata kama hamjawahi kuonana hata siku moja, haichukui hata masaa mengi, tayari wote mnakuwa kama mmezaliwa pamoja," alisema mchezaji huyo a mbaye pia huichezea Zanzibar Heroes.

Alisema kitu kingine kitakachomfanya kuwa na mzuka wa kufunga ni aina ya mashabiki wa Mashujaa ambao wanaipenda mno na kuishangilia timu yao kwa mbwembwe kila inapocheza hasa kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Lake Tanganyika.

"Nimeona mashabiki wana mzuka kweli na timu yao, wana moyo na timu yao, hata nilipoona Mashujaa wanashika nafasi ya tatu kwa kuingiza mashabiki wengi uwanjani nyuma ya Simba na Yanga sikushangaa ni kitu kizuri sana, hii inatuongezea moyo hata sisi wachezaji kupambana," alisema

Karihe pia amewahi kuzichezea klabu za Mafunzo FC ya Zanzibar, Ruvu Shooting, Azam FC, Lipuli, Mbeya City na Dodoma Jiji kabla ya kujiunga na Mtibwa Sugar.

# Michezo



Jumapili Julai 28, 2024
Nipashe

Man City yataja bei ya Alvarez UKURASA 21

# Simba SC yatua kwa Horoya kumsajili mbadala wa Lakred

## ●●● Ni golikipa wa timu ya taifa ya Guinea, yapambana kumtangaza siku ya...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetajwa kuwa kwenye mazungumzo na Horoya FC ya nchini Guinea kwa ajili ya kumsajili golikipa wa timu hiyo Moussa Camara anayeichezea pia timu ya taifa hilo ili kuziba nafasi ya Ayoub Lakred ambaye ameumia mazoezini na kutarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa angalau wiki nne mpaka sita.

**Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa Simba inataka dili hilo likamilike kabla ya kilele cha tamasha lao la kila mwaka la 'Simba Day' Agosti 3, ili kipa huyo mwenye miaka 25, awe mmoja wa wachezaji watakaotambulishwa.**

Mtoa taarifa amesema kuwa ingewezekana kumsubiri Ayoub, lakini inaona mechi nyingi muhimu ambazo ni za Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Tanzania na mechi za hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika zitachezwa mapema zaidi na haitaki kufanya makosa kama ya msimu uliopita ya kusubiri wachezaji wapone au wawe fiti.

"Ukweli ni kwamba Ayoub hayupo fiti kudaka kwa siku za hivi karibuni, kwanza licha ya kuumia na madaktari kusema anaweza kupona baada ya wiki nne mpaka sita, lakini ameongezeka sana uzito, kutokana na hilo hata kama atarudi ndani ya muda huo bado hatokuwa fiti, kwa sababu anatakiwa aanze tena mazoezi kwa ajili ya kujiweka fiti, kimahesabu anaweza kukaa hata miezi miwili, watu hawawezi kusubiri hilo kwa sababu tuna michuano mingi mikubwa na muhimu ambayo tunatakiwa tuanze vizuri ", alisema mtoa taarifa ndani ya Simba.

Inaelezwa iwapo dili hilo litafanikiwa, Simba inaweza kukata jina la Ayoub kwenye usajili wa Ligi Kuu na nafasi yake kuchukuliwa na Camara kwa sababu kanuni inataka wachezaji wa kigeni 12 tu, lakini likiachwa katika mechi ya kimataifa hadi kipindi cha dirisha dogo watakapoamua vinginevyo.

Kama Camara atafanikiwa kutua nchini atakuwa kipa wa pili kusajiliwa nchini kutoka Horoya ya Guinea kwani tayari klabu ya Singida Black Stars imemsajili golikipa Mohamed Kamara kutoka klabu hiyo hiyo.

Tofauti yao ni kwamba kipa wa Singida Black Stars anaichezea timu ya taifa ya Sierra Leone na wa Simba yuko kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Guinea.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema pamoja na kuwatambulisha wachezaji wapya, lakini bado hawajamalizia usajili, hivyo chochote kinaweza kutokea.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kwenye tamasha la kilele cha Simba Day kwani kuna 'sapraizi' za nguvu.

"Sisi hatujamaliza, chochote kinaweza kutokea wakati wowote kwa hiyo nawataka wanachama na mashabiki wa Simba wajitokeze Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya burudani, soka na pia kuwaona wachezaji wao wapya waliosajiliwa, na wanaweza kupata 'sapraizi' nyingine ya mchezaji ambao hawajamsikia kabisa," alisema Ahmed.



Moussa Camara

## Gamondi, Nabi kuonyeshana ubabe leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Mabingwa wa Tanzania Bara Yanga wakitarajiwa kucheza leo jioni dhidi ya wenyeji wao Kaizer Chief kwenye Uwanja wa Bloemfontein nchini Afrika Kusini, katika mechi ya Kombe la Toyota, mashabiki wengi wa soka wanatarajia mpambano mwingine wa mbinu na ufundi kutoka kwa makocha Miguel Gamondi na Nasreddine Nabi.

Mashabiki wengi Tanzania na Afrika wanataka kuona makocha hao waliojaliwa mbinu za ufundishaji na ufundi nani ataibuka mbabe wa mwenzake.

Vita ya makocha hao inakuja kutokana na Nabi raia wa Tunisia kuwahi kuifundisha Yanga na alipotoka nafasi yake ikachukuliwa na Gamondi raia wa Argentina.

Makocha hao kwa nyakati tofauti wameipa mafanikio klabu hiyo katika kipindi kifupi walichokaa na timu.

Nabi mbali na kuwapa ubingwa wa Ligi Kuu Yanga kwa misimu miwili mfululizo, pia aliifikisha timu hiyo hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika huku Gamondi akifanikiwa kuipa ubingwa wa Ligi kuu msimu uliopita na kuifikisha kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nabi aliyeifundisha Yanga kuanzia mwaka 2021 hadi 2023, akitokea Al Merrikh ya Sudan, kwa sasa ndiye Kocha Mkuu mpya wa Kaizer Chiefs, akijiunga nayo akitokea FAR Rabat ya Morocco ambayo alitua mara tu baada ya kuondoka Yanga.

Gamondi ndiye aliyechukua mikoba yake Yanga akitokea IR Tanger ya Morocco, na moja kwa moja akaiwezesha Yanga kutinga hat-

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042